**WANAOTOA** taarifa bila ya kufuata utaratibu waonywa

UKURASA 2



**TMDA** yafafanua usalama wa barakoa zinazoshonwa mitaani

UKURASA 3




UKURASA 11


# Nipashe

Jumamosi Machi 6, 2021 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • Na. 0580511

www.ippmedia.com

The Guardian digital · nipasheTZ · nipasheTZ · nipasheTZ · 0745 700710


# INATISHA

**MAMIA** wapima maradhi ya moyo JKCI, asilimia 80 wakutwa na presha ya juu...*Endelea Uk. 2*



## SERIKALI YATANGAZA KUWALIPA FIDIA WALIOPISHA MRADI SGR

UKURASA 2

Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, akikagua ujenzi wa Reli ya Kisasa (SGR) inayojengwa na kampuni ya Yapi Markezi, kipande cha Ihumwa- Igandu, ikiwa ni sehemu ya pili ya mradi huo kutoka Morogoro hadi Makutupora mkoani Dodoma, jana. **PICHA: OWM**

# Gwajima anusa ufisadi upanuzi hospitali

UKURASA 3

**MICHEZO** SIMBA YAJIPANGA KUKAMILISHA KAZI UK. 24

MAONI, KATUNI UK. 6

# Mamia wakutwa na presha ya juu

**Na Romana Mallya**

WATU 561 wamepimwa viashiria vya magonjwa ya moyo na kati yao, asilimia 80 wamekutwa na shinikizo la juu la damu huku asilimia 30 walikuwa hawajui kama wana tatizo hilo na kuanzishiwa matibabu.

Upimaji huo ulifanywa kwa siku mbili kuanzia juzi wilayani Temeke mkoani Dar es Salaam na kuhusisha wataalamu wa magonjwa ya moyo wanawake kutoka Taasisi ya Moyo ya Jakaya Kikwete (JKCI).

Kwenye kiwanja cha Zakhem, kulikofanyika upimaji huo, Mwenyekiti wa Wanawake wa JKCI, Anjela Muhozya, aliwaambia waandishi wa habari wamefanya upimaji huo ikiwa ni sehemu ya maadhimisho ya Siku ya Wanawake Duniani.

Dk. Muhozya ambaye ni Daktari Bingwa wa Usingizi na Wagonjwa Mahututi, alisema asilimia 50 ya waliopimwa, walikuwa wanajua wana tatizo, lakini hawakuendelea na matibabu kutokana na sababu mbalimbali.

"Asilimia 40 ya waliokutwa na matatizo, walikamilisha huduma ya matibabu viwanjani hapa kwa kupewa dawa na ushauri na asilimia 20 walipewa rufani kwenda kutibiwa katika Taasisi ya JKCI na Hospitali ya Rufani Temeke," alisema. Dk. Muhozya ambaye ni Mkurugenzi wa Upasuaji katika taasisi hiyo, alisema kati ya watu waliowapima, asilimia 10 hawakuwa na tatizo lolote la kiafya, lakini uzito wao ulikuwa mkubwa.

Alisema walitumia upimaji huo kutoa elimu ya lishe bora kwa wananchi ili kuepukana na maradhi hayo ya moyo. Mkuu wa Wilaya ya Temeke, Godwin Gondwe, aliwashukuru wataalamu hao na kubainisha kuwa wananchi wameokoa fedha ambazo wangelipia hospitalini kupata huduma hiyo.

Gondwe alisema wilaya yake itaendelea kushirikiana na JKCI katika kuhakikisha wananchi wanafikiwa na wataalamu wa taasisi hiyo. Mkurugenzi Mtendaji wa JKCI, Prof. Mohamed Janabi, alisema JKCI itahakikisha wananchi wengi zaidi wanafikiwa na huduma za matibabu ya kibingwa na elimu ya magonjwa hayo.

Alisema amefika kwenye viwanja hivyo ili kuwaunga mkono wanawake wa taasisi wanaofanya upimaji huo kwa wananchi.



Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk. Hussein Ali Mwinyi, akizungumza na wafanyabiashara waagizaji bidhaa za vyakula kutoka nje, Ikulu jijini Zanzibar jana. **PICHA: IKULU**

# Majaliwa: Waliopisha SGR watafidiwa

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa, amekagua kipande cha pili cha ujenzi wa reli ya kisasa (SGR) cha Morogoro hadi Makutupora, Singida ambao umefikia asilimia 56.6, huku akiwahakikishia wananchi walioachia maeneo yao kupisha mradi huo kuwa wote watalipwa fidia zao.

Akikagua jana kipande cha Ihumwa hadi Igandu kinachojengwa na Kampuni ya Yapi Merkezi, Majaliwa alisema ameridhishwa na kasi ya ujenzi huo na kubainisha kuwa hakuna mwananchi aliyepisha mradi huo atakayepoteza haki zake.

Alibainisha kuwa Rais John Magufuli ameamua kuboresha miundombinu mbalimbali ya usafiri nchini ikiwamo SGR ili kurahisisha usafirishaji wa abiria na mizigo. Alisema kukamilika kwa mradi huo kutaongeza ufanisi wa usafirishaji wa abiria na mizigo kwa kupunguza muda wa safari kutoka Dar es Salaam hadi Dodoma ambapo muda utakuwa saa tatu badala ya saa nane za sasa kwa usafiri wa basi.

Aliwataka Watanzania waliopata kazi katika mradi huo, kufanya kazi kwa uaminifu na weledi wa hali ya juu, ili kuudhihirishia ulimwengu kwamba Watanzania wanaajirika. Kuhusu usafiri wa anga, Majaliwa alisema ndege tatu zinatarajiwa kuwasili nchini muda wowote ili kuwa na ndege 11.

Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Reli (TRC), Masanja Kadogosa, alisema ujenzi huo umegawanyika katika vipande vitano ambapo kipande cha Morogoro hadi Makutupora chenye urefu wa kilomita 422 kinatarajiwa kukamilika Februari mwakani.

Alisema mkataba huo umeongezwa muda na ujenzi wake unagharimu Sh. trilioni 4.4 ambapo hadi sasa mkandarasi amelipwa Sh. trilioni 1.8.

"Ujenzi wetu upo asilimia 56.6. Katika mchanganuo, kazi ya ununuzi wa malighafi ya ujenzi ipo zaidi ya asilimia 92, kazi ya uzalishaji wa zege asilimia 73.4, utandikaji wa reli tupo asilimia 33.4, uchorongaji mahandaki umekamilika kwa asilimia 100, madaraja asilimia 61, ujenzi wa vivuko vya watu asilimia 67, vya mifugo asilimia 83.3, makalavati asilimia 71.3, stesheni asilimia 46.75," alisema.

Vilevile, alisema katika ujenzi wa stesheni za mizigo, wamefikia asilimia 49.1, ujenzi wa nguzo za umeme asilimia 33, vituo vya kupooza umeme asilimia 33, ujenzi wa mfumo wa mawasiliano asilimia 31. Kuhusu ajira, alisema watu 8,014 wameajiriwa kwenye kipande hicho. Kati yao, asilimia 81 ni Watanzania huku asilimia 19 wakiwa ni raia wa kigeni.

Kadogosa alisema mkandarasi pia ametoa kazi zenye thamani ya Sh. bilioni 545 kwa kampuni za Tanzania na Sh. bilioni 485 amelipa kodi na tozo mbalimbali.

Alisema ujenzi wa kipande cha kwanza cha Morogoro hadi Dar es Salaam umefikia zaidi ya asilimia 90 ambapo sasa kuna umaliziaji unafanyika wa vipande vidogo.

Awali, Mbunge wa Mvumi, Livingstone Lusinde, aliomba serikali kuwalipa fidia wananchi walioachia maeneo yao ili kupisha mradi huo, akibainisha kuwa hadi sasa bado hawajalipwa fidia tangu wafanyiwe tathmini miaka mitatu iliyopita.

"Kuna baadhi ya wananchi hawajalipwa fidia ya maeneo yao. Ni miaka mitatu sasa tangu ifanyike tathmini.

"Tulikuwa na shule ikabomolewa lakini imetolewa fidia ya Sh. milioni 168, haiwezi kutosha kujenga shule nyingine, tunaomba tuongezewe fedha kama itashindikana basi wabaki na hizo fedha sisi watujengee shule," alisema.

# Wanaotoa taarifa kinyemela waonywa

**Na Grace Semfuko,** MAELEZO

KATIBU Mkuu wa Wizara ya Habari, Sanaa, Utamaduni na Michezo, Dk. Hassan Abbasi, amewaonya watu na vyombo vya habari vinavyokiuka taratibu za utoaji wa taarifa kwa jamii kuhusu mambo mbalimbali ya serikali.

Licha ya kutoa onyo, amesisitiza kuwa ziko mamlaka zilizothibitishwa kwa ajili ya utoaji wa taarifa hizo.

Dk. Abbasi ambaye ni Msemaji Mkuu wa Serikali, alisema hayo jana kuwa katika siku za hivi karibuni kumekuwa na tabia mpya ya baadhi ya vyombo vya habari, watu na mitandao ya kijamii kutoa taarifa mbalimbali zinazohusu serikali na taasisi zake bila kuzingatia misingi ya utoaji wa taarifa hizo. Alisema jambo hilo ni kinyume cha matakwa ya sheria na kuwataka kuacha hufanya hivyo.

"Kuna tabia mpya imejitokeza ya baadhi ya watu, mtu anajitokeza anaanza kutoa takwimu zake kuhusu maradhi mbalimbali, vifo na wagonjwa. Kwa niaba ya serikali, ninaomba kusisitiza si sahihi na tuviombe vyombo vya habari viachane kabisa na watu wa namna hiyo.

"Asasi za kijamii mbalimbali, viongozi wa dini, wa siasa, kila mwanajamii anapaswa kushiriki katika kutoa elimu kuhusu hatua za kuepukana na kuhamasisha kuitoa jamii hofu na kusisitiza masuala yale ambayo yapo kwenye miongozo lakini masuala ya takwimu na kisera yanapaswa kubaki kwa serikali," alisema.

Dk. Abbasi alisema serikali imekuwa ikitoa taarifa zake kwa kuzingatia taratibu na kwamba yeyote anayehitaji taarifa zozote za serikali, milango iko wazi na kwamba awasiliane mamlaka husika ili kupata taarifa sahihi za takwimu anazotaka kuzitoa.

"Hivi karibuni Mheshimiwa Rais (John Magufuli) aliagiza viongozi mbalimbali watoe taarifa kwa umma waeleze miradi na matukio mbalimbali yanatokea katika taasisi zao. Nimeona leo (jana) nisisitize tena kwamba serikali ina utaratibu wake wa kutoa taarifa," alisema.

Pia alisisitiza kuwa utoaji wa taarifa zinazohusu maslahi ya umma kama magonjwa mbalimbali yakiwamo ya milipuko na mengineyo, ni kazi ya serikali na si mtu binafsi.

"Kwa hiyo watu wengine ambao hawahusiki na taratibu hizo hawapaswi kuingilia huo mfumo na hiyo itifaki kama ilivyo kwenye maeneo mbalimbali. Mfano kwenye maeneo ya magonjwa ya kuambukiza, magonjwa ya mlipuko, ziko taratibu za Sheria ya Huduma na Sheria ya Afya ya Jamii, zimeeleza wazi kabisa kwamba ni kiongozi wa nafasi gani anaweza kutoa taarifa.

"Kwa mfano mwaka jana, Tanzania ilipopata ugonjwa wa Corona, Mheshimiwa Rais alitoa itifaki ya viongozi watakaosemea ugonjwa huo. Sasa mtu anapoibuka na kusema anakosea," alisisitiza.

Hata hivyo, Dk. Abbasi aliwataka watu kuendelea kuchukua tahadhari za kujikinga na maambukizi ya ugonjwa huo.

## HABARI KITAIFA

# TMDA yatoa ufafanuzi usalama barakoa zinazoshonwa mitaani

**Na Mary Geofrey**

BARAKOA zinazozalishwa mtaani kwa kutumia kanga, vitenge na aina nyingine za vitambaa ni salama kwa zaidi ya asilimia 90, imebainishwa.

Ofisa Ukaguzi wa Maabara wa Mamlaka ya Dawa na Vifaa Tiba (TMDA), Obson Julias, alibainisha hayo alipozungumza na waandishi wa habari katika ofisi za mamlaka hiyo mkoani Dar es Salaam jana.

Alisema barakoa zinazozalishwa na wajasiriamali, zimefanyiwa vipimo na kubainika zina uwezo wa hadi asilimia 99 ya kukinga maambukizi yatokanayo na bakteria wanaoambukiza corona.

"Hapa tunapima barakoa kubaini ubora wake kama zinafaa kwa matumizi ya kujikinga na vimelea. Kwa barakoa ambazo zinatengenezwa na wajasiriamali wadogo na majumbani, zina usalama kwa sababu tumezifanyia vipimo na kujiridhisha na usalama wake," alisema.

Alitaja aina hizo za barakoa ni zile ambazo zinashonwa majumbani kwa kutumia nguo na vitambaa safi na salama.

Alisema kuwa katika maabara hiyo, wanapima barakoa kuangalia ubora kama inaweza kupenyeza bakteria, kama ina uwezo wa kupitisha hewa safi na usafi wa barakoa.

"Barakoa huwezi kutambua ubora wake hadi ipimwe maabara, lakini vipimo ambavyo vya kawaida ni kujua kama ni safi na yenye uwezo wa kupitisha hewa safi," alisema.

Meneja wa Mawasiliano na Elimu kwa Umma wa TMDA, Gaudencia Simwanza, alisema wamekuwa wakichukua barakoa zinazozalishwa kutoka wauzaji na kuzipima ubora wao na asilimia kubwa ni salama na hazina vimelea vya corona.

Alisema wanapokea bidhaa za barakoa kutoka nje ya nchi na zinazozalishwa nchini ambazo asilimia kubwa zimekidhi ubora wa kuanzia asilimia 70 vinavyokubalika.

# Gwajima anusa ufisadi mradi upanuzi hospitali

**Na Julieth Mkireri,** KIBAHA

WAZIRI wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Dk. Dorothy Gwajima (pichani), amenusa harufu ya ubadhirifu katika mradi wa upanuzi wa Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Pwani ya Tumbi ambao umekwama kwa miaka 10 sasa.

Katika ripoti aliyopewa na Katibu Tawala wa Mkoa wa Pwani, Delphine Magere, Dk. Gwajima alishangazwa na ongezeko la fedha kutoka Sh. bilioni tano hadi Sh. bilioni 29.

Dk. Gwajima alishtushwa na taarifa hiyo jana mjini hapa alipofanya ziara ya kufuatilia utekelezaji wa maagizo yake aliyoyatoa Desemba 24, mwaka jana, alipotembelea hospitali hiyo kukagua huduma zinazotolewa na upanuzi wa majengo.

Kutokana na hali hiyo, ametoa siku 30 kwa Katibu Tawala Mkoa wa Pwani, Delphine Magere, kusimamia kamati inayofuatilia mradi huo.

"Leo (jana) nimepokea taarifa ya katibu kawala niliyomwelekeza kufuatilia na kufanya tathmini katika uboreshaji na upanuzi wa majengo. Sasa natoa tena siku 30 ifanyike tathmini ya kina kwenye mradi huu baada ya hii ya awali kuonyesha mapungufu (upungufu) na hasara " alisema.

Waziri Gwajima alisema ripoti aliyokabidhiwa ilionyesha upotevu wa Sh. bilioni 1.6 pia mkanganyiko wa makandarasi wawili katika mradi huo ambao ni SUMA JKT na Must Construction Bureau.

"Ifanyike tathmini ya kina kwa mradi mzima siku zisizozidi 30 rejeeni katika vipimo vya jengo zima. Kamati pia ihakiki uhalali wa Sh. bilioni 29 wakirejea mpango wa upanuzi wa majengo zibainishwe sababu za ongezeko za fedha hizo kutoka Sh. bilioni tano," alisisitiza.

Gwajima alisema katika taarifa ya upanuzi wa majengo hayo, makadirio yaliyofanywa na mkoa yalilenga kutumia Sh. bilioni tano kabla ya serikali kuonyesha nia ya kufanya upanuzi katika mradi huo ambao mapendekezo yalielezwa kuwa ni Sh. bilioni 29 badala ya ile ya awali kwa majengo hayo.

Katibu Tawala Mkoa wa Pwani Delphine Magere alisema amekabidhi ripoti hiyo ambayo imeeleza fedha zilizotolewa na serikali zilivyotumika na upotevu uliobainika.

Magere alisema serikali na wadau wamechangia Sh. bilioni 9.4 kwa ajili ya upanuzi wa majengo hayo na kwamba hadi sasa Sh. bilioni 5.5 zimetumika.

Alisema katika fedha zilizotumika, hakuna uhalisia wa thamani ya fedha na kwamba upotevu uliobainika ni upande wa sampuli ya vipimo na si mradi mzima.

"Ripoti ya awali tuliyoikabidhi imeonyesha malipo hewa ambayo hayakufuata taratibu. Sasa tunakwenda kufanya tathmini kugusa mradi mzima na ripoti yetu itaonyesha uhalisia wa hasara iliyobainika.

"Kwa siku 30 tulizopewa tutakamilisha kwani mapungufu (upungufu) mengi (mwingi) tumeshabaini na sasa tutakamilisha kwa wakati," alisema Magere. Mganga Mkuu wa Mkoa wa Pwani, Dk. Gunini Kamba, alisema pamoja na kuchelewa kukamilika mradi huo, ulazima wa upanuzi bado upo.



Alisema michoro ya awali ilishapitwa na wakati na kwamba itachorwa mipya na huku akibainisha kwamba upanuzi utakapokamilika, huduma za kisasa zaidi zitatolewa katika hospitali hiyo.

Mhandisi wa Mkoa wa Pwani ambaye ni Msanifu wa Majengo, Paul Korosso, alikiri kuwapo na mkanganyiko wa makandarasi wawili katika mradi huo na kwamba jambo hilo litabainika zaidi katika tathmini itakayofanywa kwa siku 30.


## BANI INVESTMENT LIMITED

## TANGAZO LA MNADA

Kwa idhini tuliyopewa na **Benki ya NCBA Tanzania**, tutauza kwa mnada wa hadhara mali zilizowekwa kama dhamana ya mkopo. Mnada utafanyika mahali zilipo mali hizi, siku na saa kama ilivyoonyeshwa katika jedwali lifuatalo:

| JINLA MDAIWA/ MMILIKI | MALI ILIYOWEKWA DHAMANA | MAHALI ILIPO | TAREHE | MUDA |
|---|---|---|---|---|
| AHMED HUSSEIN ABDUKARIM / AH ENTERPRISES | Nyumba ya kuishi yenye CT No. 102971, Kitalu Na."B" Kiwanja Na.1707. | Kinyerezi-Dar es salaam | 20.3.2021 | 4:00 asubuhi nakuendelea |
| PASTORY KYOMBA/VAILETH ELIUD KUJU | Nyumba ya kuishi yenye CT No. 78577, Kitalu Na."N" Kiwanja Na.79. | Tabata-Dar es salaam | 24.3.2021 | 4:00 asubuhi nakuendelea |

**MASHARTI YA MNADA**

1. Nyumba zitauzwa "kama zilivyo " as is where is basis"
2. Mnunuzi atakayeshinda atalipa malipo ya awali ya 25% ya bei ya mnada siku ya mnada na 75% katika muda wa siku 14.
3. Mnunuzi atakayeshindwa kumalizia salio la 75% katika muda uliopangwa hapo juu hatarudishiwa fedha alizolipa awali na mnada utarudiwa siku nyingine itakayopangwa.
4. Gharama zote za kubadilisha hati miliki ni juu ya mnunuzi
5. Wateja wote mnakaribishwa kuona na kukagua nyumba muda wote isipokuwa usiku.

**Kwa maelezo zaidi wasiliana na Ofisi ya:**
**BANI INVESTMENT LTD, P.O. Box 71340 Dar es Salaam LIDA Building 3rd floor office No. 0313 Nkrumah Street Tel: 0713 224 578, 0718 384 796**

## SUKAH SECURITY CO. (T) LTD
### AUCTION MART & COURT BROKER
(WATU WA KAZI)

HEAD OFFICE: P.O. Box 10751, DVN Building, Posta Road Mwanza. Mob: 0754 860 435, 0715 860 435

Dealers in: Day and Night Safe Guards, Security Consultants, Rapid Ambulance response, Dog Unit and Mobile Patrolling, Debt collector and General Auctioneers

KAGERA BRANCH: P.O. Box 574, Mobile: 0754 860 435 KARAGWE.

## NOTISI / TANGAZO LA MNADA

KWA IDHINI TULIYOPEWA NA **NCBA BANK SUKAH SECURITY AUCTION MART** TUNATANGAZA KUUZA DHAMANA ZA WADAIWA SUGU WALIOSHINDWA KULIPA MIKOPO YAO KATIKA BENK TAJWA HAPO JUU KAMA WATASHINDWA KULIPA MADENI YAO NDANI YA SIKU (14) TANGU KUTOLEWA KWA TANGAZO HILI. MINADA ITAFANYIKA KAMA INAVYOONESHA KWENYE JEDWALI HAPO CHINI

| NA. | JINA | DHAMANA | TAREHE | MUDA |
|---|---|---|---|---|
| 1 | GEORGE LUGEMBE MALYETA | PLOT NO. 320,BLOCK 'A' KABUHORO | IJUMAA 19/03/2021 | SAA NNE ASUBUHI |
| 2 | KARAMA SALEH MANSOOR | PLOT NO. 43, BLOCK 'AII' KIRUMBA AREA | IJUMAA 19/03/2021 | SAA TANO ASUBUHI |
| 3 | MATHEW SIMON | PLOT NO. 71 KIRUMBA VALLEY | IJUMAA 19/03/2021 | SAA SITA MCHANA |
| 4 | JAROME MWASHA | PLOT NO. 254, BLOCK 'A' KISEKE AREA | IJUMAA 19/03/2021 | SAA NANE MCHANA |
| 5 | HEMED HAMIS RAMADHAN | PLOT NO. 3, BLOCK 'A' MIHAMA AREA | JUMAMOSI 20/03/2021 | SAA NNE ASUBUHI |
| 6 | PAMELA MAKEIRA MARUBA | PLOT NO. 408, BLOCK 'B' NYEGEZI | JUMAMOSI 20/03/2021 | SAA SITA MCHANA |
| 7 | HIPOLITE KILOSARA NDAMALYA | PLOPT NO. 20, BLOCK'C' | JUMAMOSI 20/03/2021 | SAA NANE MCHANA |
| 8 | EMMANUEL TEMBA NG'OLLO | PLOT NO. 23, BLOCK 'B' MISUNGWI | JUMAPILI 21/03/2021 | SAA NNE ASUBUHI |
| 9 | GIKURU COMPANY LTD | PLOT NO. 160, BLOCK 'Q' CENTRASL AREA | JUMAPILI 21/03/2021 | SAA SITA MCHANA |
| 10 | BANYANGA AUTO GLASS LTD | PLOT NO.119, BLOCK 'F' NYEGEZI AREA | JUMAPILI 21/03/2021 | SAA NANE MCHANA |

-*********MASHARTI YA MNADA**

MNUNUZI ANATAKIWA KULIPA 25% PAPO HAPO NA 75% BAADA YA SIKU KUMI NA NNE (14)

***NYOTE MNAKARIBISHWA***

**KWA MAWASILIANO: 0754-860435/ 0767-372515**

## STANBIC BANK TANZANIA

**IN THE HIGH COURT OF TANZANIA**

**(COMMERCIAL DIVISION)**

**AT DAR ES SALAAM**

**COMMERCIAL CASE NO. 23 OF 2020**

**STANBIC BANK TANZANIA LIMITED ............................ PLAINTIFF**

**VERSUS**

**DEOGRATIUS BONIPHACE KIGALU ............................DEFENDANT**

**DECREE:**

**WHEREFORE,** the Plaintiff prays for judgment and decree against the defendant jointly and severally as follows:-

(a) Payment of TZS 79,195,296.59 to be paid by the Defendant as pleaded in paragraphs 4 and 7 of this plaint.

(b) Interest on the sum stated at (a) above at the rate of 25% per annum from the date of filing this suit to the date of Judgment.

(c) Interest on the decretal amount at the Court's rate of 7% from the date of Judgment up to the date of payment;

(d) Costs of the suit be paid for by the Defendant.

(e) General damages to be assessed by the Court.

(f) Any other relief that this Honourable Court may deems fit and just to grant in favour of the Plaintiff.

This suit coming up for Default Judgment on 26th day of February, 2021, before Hon. Dr. D.J. Nangela, Judge in the presence of Ms. Alice Mutungi, Advocate for the Plaintiff and in the absence of the defendant.

**THIS COURT DOTH HEREBY ORDER THAT:**

The Default Judgment entered in favour of the Plaintiff as follow:-

1. The Defendant is hereby ordered to pay to the Plaintiff a sum of TZS 79,195,296.59 being the outstanding loan amount and interest thereon.
2. The Defendant is ordered to pay interest on the above sum at rate of 17% per annum, from the date of filing of this case i.e., 19th March, 2019, to the date of this default judgment (i.e., 26th February, 2021).
3. The Defendant is ordered to pay interest on decretal amount at rate of 70% from the date of this default judgment till when the decree is fully satisfied;
4. The Defendant is ordered to pay to the Plaintiff all Costs pertaining to this suit.
5. Since the Plaintiff's supporting affidavit does not offer sufficient proof regarding the prayer for general damages suffered, I decline to award general damages.
6. In terms of Rule 22(2) (a) and (b) High Court (Commercial Division) Procedure Rules, 2012 (as amended, 2019), the Court makes further orders that the decree emanating from this suit shall not be executed unless the decree holder has, within a period of ten (10) days from the date of this default judgment, publish a copy of it (the decree) in at least two (2) widely circulated news papers in the country and after a period of twenty one days (21), from the date of expiry of the said ten (10) days, has elapsed.

Given under my hand and the seal of the Court this day of 26th day of February, 2021.

THE HIGH COURT OF TANZANIA COMMERCIAL DIVISION

Dr. D. Nangela
**JUDGE, HIGH COURT OF TANZANIA**
**(COMMERCIAL DIVISION)**
26th day of February, 2021

Extracted on 26th day of February, 2021

Stanbic Bank IT CAN BE™


# Watumishi 23 wajitangaza kuwa na VVU

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

WATUMISHI 23 wa Halmashauri ya Jiji la Mbeya wanaoishi na maambukizi ya Virusi vya Ukimwi (VVU), wamejiweka wazi hali zao na kuunda umoja wao kwa lengo la kushirikiana kwenye shughuli mbalimbali.

Mwenyekiti wa Umoja wa Watu Wanaoishi na VVU Konga ya Jiji Mbeya, Douglas Kisunga, aliyasema hayo, juzi, wakati wa ziara ya Kamati ya Bunge ya Masuala ya Ukimwi, Kifua Kikuu na Dawa za Kulevya huku akibainisha kuwa umoja huo ni miongoni mwa Konga Kata 31 zilizoundwa ndani ya jiji.

Alisema kati ya watumishi hao, 16 ni wanawake na saba ni wanaume huku akiongeza kuwa wanaendelea kutoa elimu kwa watumishi wengine ambao wanaishi na maambukizi kuweka wazi hali zao kwa mwajiri wao ili wajiunge na umoja huo.

"Tunamshukuru Mkurugenzi wa Jiji, amekuwa akitupatia ushirikiano mkubwa kwenye konga yetu. Ametupatia mkopo wa Sh. milioni 15 kwa ajili ya kuendesha shughuli zetu na pia amekuwa akiusaidia umoja wa watumishi wanaoishi na VVU," alisema Kisunga.

Alisema Jiji la Mbeya lina kata 36, lakini mpaka sasa wameunda konga kata 31 ambayo ni sawa na asilimia 86 na kwamba wanaendelea na taratibu za kuunda konga kata tano zilizobaki ili kufikia asilimia 100.

Kisunga alisema konga hizo zinafanya kazi ya kuhamasisha wananchi kupima afya zao, wenye VVU kuendelea kutumia dawa na kuwafuatilia watoro wa kutumia dawa kurejea kwenye matumizi pamoja na kuanzisha miradi.

Mwenyekiti wa Watumishi wa Jiji Wanaoishi na VVU, Felician Simwela, alisema watumishi wanaoishi na maambukizi ni wengi lakini asilimia kubwa hawataki kujiweka wazi na kujiunga na umoja huo hali ambayo inasababisha ugumu kwenye mapambano dhidi ya janga hilo.

Alisema kitu kinachowafanya watumishi hao kutokuwa tayari kujiweka wazi hali zao ni kutojiamini na kuogopa kunyanyapaliwa na kubaguliwa na jamii.

"Tumekuwa tukiwezeshwa Sh. 200,000 na mwajiri wetu kwa ajili ya kuendesha shughuli zetu ikiwamo uboreshaji wa lishe. Tunawashauri na wenzetu ambao wanaishi na maambukizi kujiweka wazi na kujiunga na umoja huu ili tushirikiane kwenye mapambano," alisema Simwela.

Mratibu wa Tume ya kudhibiti Ukimwi (TACAIDS) Mkoa wa Mbeya, Dk. Masili Lutaragula, alisema mpaka sasa maambukizi katika mkoa ni asilimia 9.3 yanayoufanya mkoa huo kushika nafasi ya tatu baada ya Njombe na Iringa.

Alisema mpaka Desemba, mwaka jana, watu 114,886 sawa na asilimia 82 ya watu wote wanaoishi na VVU wanazijua hali zao, 114,330 sawa na asilimia 99.5 ya watu wote wanaoishi na VVU wako kwenye huduma ya tiba na matunzo ya ARV na asilimia 94.5 ya walioko kwenye tiba wamefikia kiwango cha ufubavu wa VVU.

Dk. Lutaragula alisema wanashirikiana na taasisi mbalimbali kwenye utekelezaji wa afua mbalimbali za Ukimwi ikiwamo Taasisi ya Henry Jackson Foundation and Medical Research Institute (HJFMRI) ambayo imekuwa ikisaidia wataalamu mbalimbali wakiwamo watunza takwimu na madaktari.

Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Masuala ya Ukimwi, Kifua Kikuu na Dawa za Kulevya, Fatma Toufiq, aliiagiza serikali ya mkoa wa Mbeya kwa kushirikiana na wadau mbalimbali kuongeza juhudi kwenye mapambano dhidi ya janga.

Aliwataka kutoa elimu kwa jamii kuacha kuwanyanyapaa watu wenye maambukizi huku akiupongeza uongozi wa Jiji la Mbeya kwa kuunda umoja wa watumishi wenye maambukizi.

Kamati ya Bunge ya Masuala ya Ukimwi, Kifua Kikuu na Dawa za Kulevya inaendelea na ziara kwenye mikoa ya Mbeya na Songwe kwa kutembelea taasisi mbalimbali.

# Serikali yataja chanzo cha vifo sangara Ziwa Victoria

**Na Elizabeth Faustine,** MWANZA

SERIKALI imetoa ufafanuzi wa kitaalamu kuhusu vifo vya samaki aina ya sangara vilivyotokea katika Ziwa victoria hivi karibuni.

Imesema tatizo hilo halikutokana na kuuliwa kwa sumu, bali vifo vyao vilitokana na kuchafuka kwa hali ya hewa ziwani.

Baada ya kutokea vifo hivyo, serikali ilichukua sampuli na kuzipima maabara na ikaonekana samaki hao hawakuuawa kwa sumu.

Katibu Mkuu wa Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Dk. Rashid Tamatamah, alibainisha hayo alipozungumza na waandishi wa habari jijini Mwanza, akisema kuwa baada ya kutokea vifo vya samaki na mizoga kuonekana ikielea, maabara ya ubora wa samaki kwa kushirikiana na Taasisi ya Utafiti wa Uvuvi Tanzania (TAFIRI), walichukua sampuli zaidi ya saba kwa ajili ya vipimo na katika hizo hakuna sampuli iliyobainika kuwa na sumu.

"Tarehe 15 Januari nilieleza hapa uwapo wa vifo vya samaki katika Ziwa Victoria upande wa Uganda na mara baada ya kuona taarifa ile, tulifanyia kazi kwa kuchukua sampuli zaidi ya saba na kuzifanyia vipimo. Kati ya hizo, hakuna hata moja iliyoonyesha kuwa na sumu," alisema.

Dk. Tamatamah alisema vifo vya samaki hao vilitokana na mzunguko wa maji katika tabaka la juu na chini kwa vipindi vya mwaka hasa Julai, Agosti na Septemba kwa sababu ya hali ya hewa na kuwataka wananchi kutowatumia samaki hao kama kitoweo.

Alisema tukio la samaki kufa katika Ziwa Victoria hutokana na mzunguko wa majira ya mwaka na kwamba samaki aina ya sangara huishi katika maji ya tabaka la kati na juu ambalo lina hewa ya kutosha ya oksijeni.

Aliongeza kuwa wanapokosa hewa, hukumbwa na matatizo mengi ikiwamo vifo hasa kwa samaki wakubwa.

"Sangara wakubwa wanahitaji oksijen nyingi, sababu kubwa ya vifo vya samaki ni mzunguko wa maji katika Ziwa Victoria maeneo machache, msiwe na wasiwasi na wananchi wasiwatumie kama vitoweo," alisema.

Januari 2 mwaka huu, walionekana samaki waliokufa katika maeneo ya Masonga-Sota Tarime, Nyamikoma Busega, Geita pamoja na Visiwa vya Misenyi, Bukoba.

# Wenye shida kupumua waondolewa hofu

**Na Mwandishi Wetu**

WATANZANIA wanaokumbwa na maradhi ya kushindwa kupumua vizuri na kubanwa mbavu, wameshauriwa wasipate taharuki kwa kuwa kuna dawa makini ya asili inayotibu ugonjwa huo.

Akizungumza jijini Dar es Salaam jana, Dk. Baraka Beneza alisema dawa ya Mwalaka inayotengenezwa na kampuni ya Altenative International Medicine imepata kibali cha Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto baada ya kuonekana kufikia viwango.

Dk. Beneza alisema dawa hiyo inapatikana kirahisi na kuna ushuhuda wa watu wengi ambao wameshaitumia na kupata matokeo chanya baada ya kupata matatizo ya kupumua, kukohoa na kubanwa mbavu.

"Hii dawa inapatikana kirahisi, ni kinga na tiba, hivyo nawashauri watu wakiona dalili za kubanwa mbavu na kushindwa kupumua vizuri, watumie dawa hii muda mfupi sana watakuwa wameshapata suluhisho," alisema.

Alisema dawa hiyo inatengenezwa kitaalamu na Alternative International Medicine kwa kushirikiana na kampuni ya MICO imewasaidia watu wengi waliokumbwa na shida ya kupumua, kukohoa na kubanwa mbavu.

"Watu wasitaharuki tena wanapopata matatizo ya aina hii badala yake waje wapate dozi hii ambayo ndani ya saa chache itakuwa imemaliza changamoto inayowakabili," alisema.

Abdalah Chondoma, ambaye aliwahi kupata tatizo la kushindwa kupumua, kubanwa mbavu na kukohoa sana, alitoa ushuhuda kuwa baada ya kunywa dawa hiyo ya Mwalaka hivi sasa maisha yake yanaendelea kama kawaida.

Alisema alipata ugonjwa huo wakati akisafiri na basi kwenda msibani na wenzake, lakini alipopatiwa dozi, hali yake imetengemaa na anaendelea na kazi zake.

"Iliponishika nilikuwa nabanwa na mbavu, napumua kwa shida sana lakini dawa hii imenisaidia sana kwasababu ndani ya muda mfupi sana kifua changu kilifunguka na nikawa napumua vizuri na maumivu yaliisha," alisema.

Alisema Watanzania wanapaswa kuchangamkia dawa hiyo kwani imewasaidia wananchi wengi waliokuwa na changamoto ya kupumua ambao wametoa ushuhuda wa walivyonufaika.

"Dawa hii imesajiliwa rasmi na wizara husika kwa namba TZ 17TM 0035 kwa hiyo serikali inatambua kwamba ni dawa nzuri inayotibu kwa uhakika na tulishaambiwa tuthamini vya ndani tusiamini kwamba kila kizuri lazima kitoke nje, watu watumie hii wajionee" alisema.

Joyce Mwamtanga, ambaye ni mjasiriamali wa vipuri Kariakoo alisema wiki tatu zilizopita alibanwa mbavu na kushindwa kupumua lakini alipotumia dawa ya Mwalaka alipata nafuu ndani ya muda mfupi.

"Kwa kweli tuthamini bidhaa zetu zinazozalishwa hapa nchini kwasababu hii dawa ya miti ya asili imenisaidia sana inanguvu kwasababu baada ya kuitumia haikupita nusu saa nikajiona wa kawaida kabisa," alisema Mwamtanga.

# Waziri awaonya wafanyakazi kujihusisha vitendo vya aibu

**Na Lilian Lugakingira,** BUKOBA

NAIBU Waziri wa Nishati, Stephen Byabato, amewaonya watumishi wa Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) kutojihusisha na vitendo vinavyotia aibu utumishi wa umma vikiwamo mapenzi kazini, ulevi wa kupindukia na kuwa na madeni yaliyopitiliza.

Badala yake amewataka wawe watiifu na kufanya kazi kwa uadilifu, kwa manufaa ya Watanzania.

Byabato alitoa onyo hilo jana wakati wa kikao na wafanyakazi wa TANESCO Mkoa wa Kagera, kilicholenga kukumbushana majukumu ya kazi na kuweka mikakati ya kuhudumia wananchi, ili kupunguza malalamiko yanayotokana na utendaji usioridhisha kwa baadhi ya watumishi.

Alisema serikali imeweka utaratibu wa wananchi kufikishiwa huduma ya umeme ndani ya siku 30 baada ya kukamilisha taratibu zote ikiwamo kufanya malipo yanayotakiwa. Pia aliwataka wananchi wenye malalamiko dhidi ya huduma zinazotolewa, kuyawasilisha ili kutafuta ufumbuzi.

"Nimefanya kikao Kagera, lakini tumekwishafanya vikao na watumishi pia katika mikoa mingine. Kumekuwa na malalamiko ya wananchi kulalamika kupata huduma zisizoridhisha. Sasa katika vikao hivi tunakumbushana nini wajibu wetu, tunasisitiza wawe na lugha nzuri zinazofurahisha na kuridhisha wateja ambao ndiyo waajiri wao," alisema.

Kaimu Meneja wa TANESCO Mkoa wa Kagera, Mhandisi Habibu Kinono, alisema wanaendelea na jitihada za kuongeza idadi ya wateja na kwamba kwa mwaka wa fedha 2020/21, mkoa unalenga kuunganishia umeme wateja 10,885 ambao ni sawa na wastani wa wateja 908 kila mwezi.

"Katika kipindi cha Julai, 2020 hadi Februari, mwaka huu, wateja 8,177 wamekwishaunganishiwa umeme, ambao ni sawa na asilimia 75.12 ya lengo la mwaka," alisema Kinono.

Meneja Miradi wa Kanda ya Ziwa kutoka Wakala wa Nishati Vijijini (REA), Mhandisi Ernest Makale, alisema serikali ina mpango wa kuhakikisha vijiji vyote vya mkoa vinapelekewa huduma ya umeme na kwamba REA awamu ya tatu mzunguko wa pili ilikuwa ianze mwishoni mwa Februari, lakini imesogezwa mbele hadi katikati ya mwezi huu.

Mhandisi Makale alisema mradi huo utanufaisha vijiji 114 katika mkoa mzima.


## NOTISI/ TANGAZO LA MNADA WA HADHARA

**BEST GROUP (T) LTD,** kwa mamlaka tuliyopewa na Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, chini ya benki ya **AKIBA COMMERCIAL BANK PLC,** tuna toa notisi ya kulipa madeni kwa wadaiwa wafuatao ndani ya siku 14 kuanzia tangazo hili,Vinginevyo, tutafanya minada ya hadhara kama ratiba inavyoonyesha.

| Na. | JINA LA MDAIWA | JINA LA MDHAMINI | DHAMANA NA MAHALI ILIPO | TAREHE YA MNADA |
|---|---|---|---|---|
| 1 | EMMANUEL GADI NKALANG'ANGO | EMMANUEL GADI NKALANG'ANGO | Nyumba ya makazi yenye Hati miliki no.180634 kiwanja no.224/34 kitalu"C" iliyopo Chang'ombe. | 20.03.2021 NA KUENDELEA |
| 2 | JOSEPHINE JAPHET LAWUO | JOSEPHINE JAPHET LAWUO | Nyumba ya makazi yenye Hati miliki no.91240 iliyopo Tabata Kisukulu. | 20.03.2021 NA KUENDELEA |
| 3 | LEONIDA CELESTINE KATATUMBA | JOHN BOSCO KATATUMBA | Nyumba ya makazi yenye Hati ya mauziano iliyopo Pugu Bombani. | 20.03.2021 NA KUENDELEA |
| 4 | HASSAN MAJARIBU LUPETO | HASSAN MAJARIBU LUPETO | Tractor Mahindra T580 DJX Lililopo Nakopi Mtwara | 22.03.2021 NA KUENDELEA |
| 5 | HADIJA HASSAN MWASHA | HADIJA HASSAN MWASHA | Nyumba ya makazi yenye leseni na. KND/MBS/KWN26/175 mtaa wa kisiwani Mwananyamala manispaa ya Kinondoni | 22.03.2021 NA KUENDELEA |
| 6 | VAILETH ERASTO TWEVE | JOSEPH BENEDICT/VAILETH ERASTO | Nyumba yenye Leseni ya Makazi iliyopo maeneo ya Kitunda Kati. | 20.03.2021 NA KUENDELEA |
| 7 | TWIGWELA IDRISSA ISMAIL | TIIGWELA IDRISSA ISMAIL | Nyumba yenye Hati ya mauziano iliyopo maeneo ya Kimara Mavurunza. | 23.03.2021 NA KUENDELEA |
| 8 | HENRY GEORGE MUNISS | HENRY GEORGE MUNISS | Nyumba ya makazi yenye Mkataba wa mauziano iliyopo Mbezi Msingwa. | 23.03.2021 NA KUENDELEA |
| 9 | BERNARD MONGI TARIMO | BERNARD MONGI TARIMO | Nyumba ya makazi yenye hati ya mauziano no.48977 kiwanja no.1295/1, 1296/1 & 1301, kitalu "A" vilivyopo Kagera Mikoroshini Dar es salaam. | 22.03.2021 NA KUENDELEA |
| 10 | MOSHI JUMANNE JUMA | MOSHI JUMANNE JUMA | NyumbayamakaziyenyeHatiyamauzianoiliyopoBunju B. | 24.03.2021 NA KUENDELEA |
| 11 | FLORA LAURENCE MSHANA | FLORA LAURENCE MSHANA | Nyumba ya makazi yenye hati ya mauziano iliyopo salasala kata ya wazo. | 24.03.2021 NA KUENDELEA |
| 12 | ARONI YASIN MPINGE | ARONI YASIN MPINGE | Nyumba ya makazi yenye Hati ya mauziano iliyopo Boko Chama | 24.03.2021 NA KUENDELEA |
| 13 | GERVACE ANDREW MWALLA | GERVACE ANDREW MWALLA | Kiwanja chenye Hati ya mauziano kilichopo maeneo ya Mgeule Buyuni. | 25.03.2021 NA KUENDELEA |
| 14 | IGNAS SABASI SHIRIMA | IGNAS SABASI SHIRIMA | Nyumba ya makazi yenye Hati ya mauziano iliyopo Wazo mtaa wa Kilima hewa. | 26.03.2021 NA KUENDELEA |
| 15 | ZAITUNI OMARY JUMA | ZAITUNI OMARY JUMA | Nyumba ya makazi iliyopo maeneo ya kivule wilaya ya ilala | 29.03.2021 NA KUENDELEA |
| 16 | WILIHELIM VICENTMTENGA | WILIHELIM VICENT MTENGA | Nyumba ya makazi iliyopo mbezi malambamawili. | 30.03.2021 NA KUENDELEA |
| 17 | CHRISTIAN FAUSTINE BUNDEWE | CHRISTIAN FAUSTINE BUNDEWE | Nyumba yenye Hati ya Mauziano iliyopo maeneo ya Kimara Matangini. | 30.03.2021 NA KUENDELEA |
| 18 | BENJAMIN PATRICK MABINZA | BENJAMIN PATRICK MABINZA | Nyumba yenye Leseni ya Mauziano Iliyopo maeneo ya Mbezi Msakuzi | 31.03.2021 NA KUENDELEA |
| 19 | BOSCO THADEI UTENGA | BOSCO THADEI UTENGA | Nyumba yenye Hati ya mauziano iliyopo maeneo ya kigezi chini Chanika. | 01.04.2021 NA KUENDELEA |
| 20 | JOHNSON ELIEZA MUKIZA | JOHNSON ELIEZA MUKIZA | Nyumba ambayo haijakamilika iliyopo Kifulu Manispaa ya Ilala. | 02.04.2021 NA KUENDELEA |
| 21 | REINFRIDA CHARLES MGUDE | REINFRIDA CHARLES MKUDE | Kiwanja ambacho hakijaka milika chenye Leseni No.TMK 044960 kilichopo Mbagala kwa Mangaya | 03.04.2021 NA KUENDELEA |

### MASHARTI YA MNADA

1. Mnunuzi atalazimika kulipa 25% ya bei ya nyumba au kiwanja papo hapo baada ya mnada kumalizika na 75% itakayobaki italazimika kulipwa ndani ya siku 14.
2. Ikiwa mnunuzi atashindwa kutimiza sharti lolote la mnada kuhusiana na malipo ya awali, hatarudishiwa pesa yoyote aliyokwishailipa.
3. Kwa mawasiliano zaidi; tupigie simu no. **+ 255 715-363537/766-309913**
4. Iwapo ndani ya siku 60 mnunuzi hajakabidhiwa nyumba benki itarudisha kiasi cha fedha kilichowekwa na mnunuzi benki bila gharama yeyote.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Kila la kheri Simba SC

**WAWAKILISHI** wa Tanzania, Simba ya jijini Dar es Salaam, leo wanatarajia kushuka dimbani ugenini Sudan kuvaana na wenyeji Al Merrikh katika mechi ya tatu ya hatua ya makundi ya mashindano ya Ligi ya Mabingwa Afrika itakayochezwa mjini Khartoum.

Mechi hiyo ni ya tatu kwa timu hizo zilizoko kwenye Kundi A, na wageni Simba watashuka uwanjani wakiwa na kumbukumbu ya kushinda mechi zake mbili zilizotangulia za michuano hiyo inayosimamiwa na kuandaliwa na Shirikisho la Soka Afrika (CAF).

Wekundu wa Msimbazi watashuka dimbani leo wakiwa na kumbukumbu ya ushindi wa mechi mbili zilizotangulia na hivyo kufikisha pointi sita zilizowaweka kwenye uongozi wa kundi hilo lenye timu za Al Ahly ya Misri na AS Vita ya Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC).

Katika hatua hiyo ya makundi, wawakilishi hao wa Tanzania ambao pia ni mabingwa watetezi wa Ligi Kuu Bara walianza hatua hiyo ugenini Mjini Kinshasa kwa kuwafunga AS Vita bao 1-0 halafu ikarudi nyumbani kuwakaribisha vigogo wa Afrika, Al Ahly ambao pia walipata matokeo kama yanayofanana na DRC.

Licha ya kuongoza kundi, Simba bado inahitaji kuendelea kupambana kusaka ushindi katika mechi ya leo na kujiimarisha kwenye nafasi za juu ambazo hutoa timu itakayosonga mbele katika hatua inayofuata ya mashindano hayo ambayo ni kucheza robo fainali.

Matokeo ya ushindi leo yatawaweka Simba mguu mmoja ndani kuelekea hatua ya robo fainali huku wakibakiwa na mechi nyingine tatu mkononi.

Wawakilishi hao wa nchi walifika hatua ya robo fainali mwaka juzi baada ya kufikisha pointi tisa, wakishinda mechi zote tatu za nyumbani, lakini kasi waliyoanza nayo mwaka huu imeonekana ni nzuri na hawapaswi kubweteka.

Benchi la ufundi la Simba ambalo kwa sasa liko chini ya Mfaransa Didier Gomes linatakiwa kuendelea kujiimarisha ili kusaka matokeo chanya ambayo yatawasaidia kutimiza malengo yao katika michuano hiyo kwa msimu huu.

Simba inapaswa kuingia uwanjani leo ikisahau matokeo yaliyopita na kuona kwamba wana kazi moja ya kuchukua pointi tatu na wakiuona mchezo huo ni sawa na fainali, hivyo hawatakiwi kupoteza kwa ajili ya kukamilisha safari ya kwenda hatua ya robo fainali mapema.

Katika soka lolote linaweza kutokea, Simba haipaswi kuona imemaliza kazi kwa kushinda mechi mbili za kwanza na badala yake iweke mawazo kwamba ndio kazi imeanza.

Kama ilivyoingia katika mechi ya kwanza dhidi ya AS Vita, Simba inatakiwa iwaheshimu wapinzani wao Al Merrikh ambao wamepoteza mechi mbili za kwanza na leo wataingia uwanjani wakiwa makini zaidi baada ya kufahamu walipokosea kwenye dakika 180 zilizotangulia. Ili kufikia malengo hayo, Watanzania wote wanatakiwa kuungana pamoja kuiombea dua Simba kwa ajili ya maslahi ya nchi ambayo msimu ujao itatoa wawakilishi wanne katika mashindano ya CAF badala ya wawili kutokana na Wekundu wa Msimbazi kuongeza pointi.


Inafahamika wazi katika mchezo wa soka hakuna kutegemea miujiza, inaeleweka ili timu ivune matokeo mazuri ni lazima wahusika wakubali kufanya maandalizi na mikakati mizuri kulingana na mchezo husika na kubwa wachezaji kuonyesha kiwango cha juu.

Kuendelea kufanya vyema kwa Simba si kutaipatia fedha kutokana na hatua waliyofika, pia ni nafasi nyingine ya kulitangaza jina la nchi katika medani za kimataifa ambavyo wawakilishi hao walivyoamua kuweka ujumbe wa 'Visit Tanzania' kwa malengo ya kukaribisha na kuwavutia watalii.

Hakuna kisichowezekana, kwa nguvu na mikakati iliyotumika katika mechi zilizopita, Simba inaweza kuendelea kushinda na kujiweka katika nafasi bora kwenye kundi lao.

Kila la kheri Simba, Mungu ibariki Simba, Mungu ibariki Tanzania.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



Na Barnabas Maro

# Kipendacho moyo ni dawa

**KITU** anachokipenda mtu au inachokipenda roho ya mtu huwa ni kama dawa yake.

Methali hii hutumiwa kumpigia mfano mtu anayeelekea kukipenda kitu fulani sana ingawa wengine wanakiona kibaya kwani wahenga walisema "kipendacho moyo ndiyo dawa."

Je, wewe unayesoma makala haya wajua jambo lililokuvutia hata uipende timu fulani kuliko zingine? Labda nikufahamishe kwamba "kipenda roho hula nyama mbichi." Maana yake roho ikipenda huweza kula hata nyama mbichi.

Kuna makundi tofauti ya watu wenye misimamo tofauti kuhusu mapenzi yao kwa timu mbalimbali. Kwa upande mmoja watu hufurahia aina ya mchezo wa timu fulani ilhali wengine huvutiwa na baadhi ya wachezaji kwa namna wanavyocheza. Hii ni sawa na wanavyowapenda mabingwa wa mchezo wa ngumi.

Ukifuatilia ngumi utakubaliana nami kuwa mabingwa wa mchezo huo duniani walipendwa na watu wengi zaidi, kisa ni kuwapiga wapinzani wao kwa TKO kabla ya kufikia mwisho na kuhesabiwa alama za waamuzi watatu wanaotoa pointi.

Wachezaji waliopendwa zaidi na watu wengi ni kama George Formen, Mohamed Ali, Floyd 'Money' May Weather Jr na Mike Tyson, kwani walikuwa wapiganaji mahiri dhidi ya wapinzani wao.

Kwenye kandanda ndivyo ilivyo pia. Kuna wanaokwenda viwanjani kuona jinsi wachezaji mahiri wanavyocheza, pia mtindo wa timu nzima. Wengine huvutiwa na madoido (mambo au vitu vinavyofanya jambo kuwa zuri na kuvutia watu) kama vile afanyavyo Mghana Bernard Morrison wa Simba, n.k.

Nchini Tanzania timu zinazovuta Watanzania wengi zaidi ni Yanga na Simba hata kama zinacheza mikoa mingine nje ya Dar es Salaam watazamaji huzishangilia sana timu hizo ngeni mikoani mwao ilhali wachache ndio huzishangilia timu za mikoa yao! Kumbe ndio sababu wahenga walisema " Kipenda roho hula nyama mbichi."

Sasa tuje kwenye Ligi Kuu, hasa mchezo wa Alhamisi iliyopita kati ya Coastal Union (Mmbwa Mwitu) na Yanga ya Wananchi, mchezo uliochezwa katika Uwanja wa Mkwakwani jijini Tanga.

Kama mlivyoona na kusikia, husemwa " Mgeni njoo mwenyeji apone" au " Mgeni hawezi kuuona mwezi." Hii ni methali ya kutumiwa kutukumbusha kwamba mtu ambaye ni mgeni mahali fulani hawezi kuzifahamu tabia na desturi za wenyeji mpaka aishi nao kwa muda mrefu.

Yanga iliyocheza michezo 21 bila kufungwa ilipoteza mchezo wao wa 22 kwa kufungwa na wenyeji wao ambao mara kwa mara huwapa shida sana wachezapo kwenye uwanja huo. Hao si wengine bali ni Coastal Union wanaojiita 'Mmbwa Mwitu.' Yanga walicheza kama wanaojifunza kucheza kandanda kwenye mji wa watu huku Coastal Union wakiwa walimu wao uwanjani!

Ikiwa imecheza michezo 21 bila kufugwa, ilikutana na 'walimu' wao waliowachezesha nusu uwanja kwa muda mrefu na kuumiliki mpira walivyotaka huku Yanga wakicheza kama wanafunzi wa kandanda kwa kubutuabutua tu!

Lahaula! Watapita kwa mnyama Simba? Watapita kwa Azam FC, Namungo, Biashara United n.k.? Kwa mchezo waliocheza dhidi ya 'Mmbwa Mwitu' wajiandae kukutana na kipigo cha mnyama Simba aliye mfalme wa wafalme nchini na anga za juu.

Nashindwa kueleza zaidi kwani mchezo wa kandanda una namna tatu: kushinda, kushindwa, sare au suluhu, yaani kutofungana kabisa.

Kuna minong'ono inayoenea mitaani kwamba ni kwa nini Simba wanashangilia sana kipigo cha Yanga. Simba wana sababu mbili kubwa. Kwanza "Mmbwa mwitu" yaani Coastal Union ni ndugu zao kwa hiyo wana haki ya kuwacheka Yanga. Pili ni kwa sababu hao wanyama wenzao ni timu ya Tanzania.

Je, wale wanaozishangilia timu za nje wanapozifunga timu za Tanzania wanajua wanachofanya kama si kujicheka wenyewe na kujifanya wapumbavu kwa wageni?

**marobarnabas@yahoo.com 0784334096**

## Ndikilo ashangazwa ugumu ulipaji bili

**Na Julieth Mkireri,** KIBAHA

MKUU wa Mkoa wa Pwani, Mhandisi Evarist Ndikilo, amesema ulipaji wa bili za maji katika mkoa bado ni tatizo hali inayosababisha baadhi ya maeneo miradi ya maji kufa na kusababisha ukosefu wa huduma hiyo.

Ndikilo alibainisha hayo jana alipokuwa katika kikao cha wadau wa sekta ya maji vijijini mkoani hapa kilichoandaliwa na Wakala wa Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini (RUWASA).

Alisema katika Wilaya za Rufiji na Kibaha (Halmashauri ya Wilaya ya Kibaha), iko miradi ya maji imekufa kutokana na wananchi kushindwa kulipa bili kwa wakati.

"Ulipaji wa bili za maji kwa mkoa wetu bado ni tatizo. Wananchi wanafikiri huduma ya maji ni bure na kama kuna eneo tunafeli, basi ni hili tunatakiwa kutambua kuwa maji ni bidhaa kama ilivyo bidhaa nyingine tulipie ili tuendelee kunufaika nayo," alisema.

Ndikilo alisema wananchi na taasisi wanatakiwa kulipa bili za maji kwa wakati ili huduma iwe endelevu na inapotokea hawalipi inasababisha kukwama kwa miradi hiyo na kukosa nguvu ya kujiendesha. Aidha, alisema suala la ulinzi wa vyanzo vya maji ni jukumu la kila mmoja hivyo isiachiwe RUWASA pekee kwa kuwa wanufaika ni wananchi ambao baadhi yao wanaishi karibu na vyanzo hivyo.

Mkuu huyo wa mkoa aliwaagiza wakurugenzi na wenyeviti wa halmashauri katika mkoa, kutumia mabaraza ya madiwani kujadili utengaji wa maeneo kwa ajili ya ujenzi wa ofisi za RUWASA ili kuwaondolea kero iliyopo sasa.

Katika hatua nyingine, Ndikilo aliziagiza RUWASA, Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Dar es Salaam (DAWASA) na Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Mafuta (EWURA) kukutana kujadili namna ya kutatua kero za bili za maji ambazo zimekuwa zikilalamikiwa na wananchi.

Meneja wa RUWASA Mkoa wa Pwani, Beatrice Kasimbazi, alisema hadi Desemba, mwaka jana, asilimia 73 ya wananchi waishio vijijini, walikuwa wanapata maji kwa asilimia 71 huku maeneo ya mijini wakipata asilimia 84.

Kasimbazi alisema kwa kipindi cha kuanzia mwaka 2019 hadi Februari, 2021, miradi 48 yenye gharama ya zaidi ya Sh. bilioni 9.8 inaendelea na utekelezaji na inatarajia kunufaisha watu 99,334.

Meneja huyo alisema katika mwaka 2021/22 Mkoa umejipanga kutekeleza miradi 65 itakayogharimu Sh. Bilioni 18.7. Mkuu wa Wilaya ya Rufiji, Luteni Kanal Patrick Sawala, alisema malalamiko kutoka kwa baadhi ya wananchi wake ni bili kubwa za maji kuliko uhalisia wa matumizi.

Kutokana na adha hiyo, Sawala aliomba usomaji wa bili za maji uangaliwe upya ili kuondoa kero za mara kwa mara zinazosababisha kuwapo kwa ugumu wa wananchi kulipa Ankara zao.

# Wanawake wapigiwa debe nafasi za kazi

**Na Joseph Mwendapole**

MASHIRIKA na taasisi mbalimbali yameshauriwa kuwapa kipaumbele wanawake kwenye nafasi za ajira kwani wamethibitisha kwamba wakipewa nafasi wanauwezo wa kuleta mabadiliko.

Hayo yalisemwa mwishoni mwa wiki jana na Naibu Makamu Mkuu wa Chuo Kikuu cha Ardhi (Taaluma), Prof. Gabriel Kassenga, wakati wa kongamano la Siku ya Wanawake Duniani lililoandaliwa na wanawake wa chuo hicho.

Prof. Kassenga alisema wanawake wengi waliopewa nafasi za uongozi, wamefanya kazi kubwa, hivyo kuondoa dhana iliyokuwapo kwamba hawana uwezo kama wanaume wakipewa nafasi.

Alisema asilimia 70 ya wafanyakazi wa chuo hicho ni wanawake na wote wameonyesha uwezo mkubwa sana kwenye nafasi zao tofauti kabisa na dhana iliyokuwapo.

"Ile dhana kwamba wanawake hawana uwezo kama wanaume, imepitwa na wakati. Kwa hiyo inapotokea nafasi za ajira, wanawake wapewe kipaumbele kwa sababu hapa kwetu wametuonyesha kwa vitendo kwamba wakipewa nafasi uwezo wanao," alisema.

Prof. Kasenga alisema ARU ina idara 13 za kitaaluma na kati ya hizo, nane zinaongozwa na wanawake na chuo kinaridhishwa na wanavyochapa kazi na kuleta matokeo makubwa kwenye idara wanazoongoza.

Mkuu wa Kitengo cha Jinsia chuoni hapo, Dk. Nelly Babere, alisema lengo la kufanya kongamano hilo ni kuonyesha nafasi ya mwanamke katika maendeleo na katika jamii ya Chuo Kikuu cha Ardhi na kwamba chuo hicho kimejitahidi kuweka usawa wa kijinsia.

Alisema chuo kimejitahidi kuweka usawa wa wanawake kwenye nafasi mbalimbali za uongozi hivyo uamuzi wowote unaofanywa unakuwa hauna ubaguzi wowote ule.

"Mambo mengi tunayofanya hapa ni shirikishi na hata wanafunzi huwa tunawashirikisha na kwenye maandamano ya leo kuadhimisha Siku ya Wanawake wanafunzi wameshirikishwa ili nao wajifunze usawa wa kijinsia," alisema.

Dk. Babere alisema idadi ya wanafunzi wa kike ilikuwa ndogo sana wakati chuo hicho kinaanza lakini kwa sasa idadi yao imekuwa ikiongezeka mwaka hadi mwaka kiasi cha kuwa sawa na idadi ya wavulana.

"Wakati tunaanza miaka ya 2000 ulikuwa unaweza kukuta darasa zima linawanafunzi wawili tu wa kike, lakini leo hii ukiangalia darasa lingine unakuta idadi ya wasichana ni kubwa kuliko wavulana," alisema.

Alitoa wito kwa wanafunzi wa kike na wa kiume kujitambua kwani wamekuwa wakikabiliana na changamoto tofauti tofauti hivyo wajielewa watavuka changamoto zinazowakabili.

Dk. Babere alisema ARU inashirikisha na jamii, serikali na jumuiya ya kimataifa kuendelea kuangalia nafasi ya mwanamke na kumlinda dhidi ya vitendo vya unyanyasaji ili aishi maisha ya staha na kuondokana na unyanyasaji na ukatili wowote.



Wanawake wafanyakazi wa Chuo Kikuu Ardhi (ARU), wakiwa kwenye maandamano ya Siku ya Wanawake Duniani, yaliyoambatana na kongamano kuhusu masuala ya maendeleo ya wanawake chuoni hapo, mkoani Dar es Salaam jana. Siku hiyo, huadhimishwa Machi 8, duniani kote. **PICHA: JOSEPH MWENDAPOLE**

# RC akemea makundi ndani ya ushirika

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

MKUU wa Mkoa wa Shinyanga, Zainab Telack, ameitaka bodi mpya ya Chama Kikuu cha Ushirika Kahama (KACU), kuacha makundi yasiyo na tija katika utekelezaji wa majukumu yao.

Amesema makundi huwagawa wakulima wa tumbaku na pamba na kwamba hatua hiyo husababisha mpasuko ndani ya ushirika.

Telack alisema hayo juzi muda mfupi baada ya kukamilika kwa uchaguzi wa bodi mpya na mwenyekiti wa chama hicho, Emmanuel Charahani.

Alisema kuna tabia ya baadhi ya viongozi wa bodi kuendekeza makundi baada ya uchaguzi kukamilika, hivyo kuwagawa wakulima na kusababisha migogoro isiyo na tija.

Kutokana na tabia hiyo, alisema serikali haitasita kuwawajibisha kisheria watakaobainika kutengeneza makundi ndani ya ushirika.

"Ushirika huu umekuwa mfano wa kuigwa nchi nzima katika kutetea maslahi ya wakulima na kujiendesha kwa faida. Nikiwa mlezi wa ushirika, sitakubali mharibikiwe ndani ya uongozi wangu kwa kulea tabia za baadhi ya viongozi wachache wasiokuwa wadilifu," alisema Telack.

Pia alisema taasisi za kifedha zimekiamini chama hicho na kukikopesha fedha ambazo zitawanufaisha wakulima wote wa pamba na tumbaku na kwamba kutengeneza makundi kutasababisha kupoteza imani kwa taasisi hizo na kushindwa kuendelea kukopesheka.

Naye Mrajisi Msaidizi wa Vyama vya Ushirika Mkoa wa Shinyanga, Hilda Boniphace, alisema sheria ya vyama vya ushirika inampa mamlaka ya kutengua uteuzi wa kiongozi yeyote atakayebainika kwenda kinyume hasa kwa kutengeneza makundi na kutoa siri za vikao vya bodi.

Alisema hatua za kisheria zitachukuliwa ikiwamo kuwavua madaraka viongozi watakapobainika kukihujumu chama hicho kwa kujinufaisha wao binafsi na kukwamisha shughuli za ushirika ili kulinda mali na maslahi ya wakulima.

Mwenyekiti wa KACU, Charahani, alisema atahakikisha anasimamia maslahi ya wakulima kwa kugawa pembejeo kwa wakati, viuatilifu na kutafuta masoko ili kuhakikisha mkulima ananufaika.

# Wataka elimu ukatili kijinsia

**Na Shaban Njia,** SHINYANGA

WAKAZI wa Kata ya Mwakitolyo katika Wilaya ya Shinyanga, wameomba serikali kupitia ofisi za maendeleo ya jamii, kuwapatia elimu ya ukatili wa kijinsia ili kujua sehemu ya kwenda kutoa taarifa baada ya kufanyiwa vitendo hivyo.

Hayo waliyabainisha juzi wakati wakizungumza na mwandishi wa habari hii aliyefika katika kata hiyo kuangalia hali ya ubaguzi wa kijinsia katika shughuli za kiuchumi.

Baadhi ya waandishi wa habari wanafuatilia masuala ya ukatili wa kijinsia kupitia mradi wa nafasi ya vyombo vya habari katika kumaliza ukatili dhidi ya wanawake na watoto unaotekelezwa na SPC kwa ufadhili wa Women Fund Tanzania (WFT).

Chausiku Manyabili, mkazi wa kata hiyo, alisema wamekuwa wakifanyiwa vitendo vya kikatili na waume zao, lakini hawatambui kama ni ukatili na kubaki kuendelea kuumia na kwamba wangekuwa na elimu hiyo ingewasaidia kutambua wapi wanatakiwa kupeleka malalamiko yao na kupata msaada.

"Sisi hatufahamu kukimbiwa na waume zetu nao ni ukatili. Tunakimbiwa sana hasa familia inapoongezeka, tunaona kawaida na hatuwezi kulalamika mahala popote pale. Laiti tungekuwa na elimu ya kutambua kwa upana dhana ya ukatili wa kijinsia, tungejitokeza kutoa malalamiko yetu," alisema.

Neema Tabu alisema watoto wadogo hasa wa kike wenye umri wa kwenda shule, wanashindwa kuhudhuria masomo kwa kukosa mahitaji kutoka kwa wazazi wa kiume ambao wanatumia muda mwingi katika shughuli za uchimbaji wa madini badala ya kuhudumia familia.

Ofisa Maendeleo ya Jamii wa Kata ya Mwakitolyo, Mussa Gongo, alisema amekuwa akishirikiana na kamati za mtaa katika kutoa elimu ya ukatili wa kijinsia, lakini wananchi wanapojitokeza na kukuta hakuna ajenda ya uchimbaji wa madini wanaondoka.

Alisema kwa siku anapokea kesi sita za wanawake kuachwa na kunyimwa matumizi na waume zao na asilimia kubwa ya kesi hizo zinatoka katika vijiji vya Mwakitolyo na Nyaligogo.

Ofisa Mtendaji wa Kata ya Mwakitolyo, Samson Lutonja, aliwataka wanawake kuacha tabia ya kukimbia mikutano ya hadhara wakati wa kutoa elimu ya ukatili wa kijinsia na kutoa taarifa ya vitendo vya kikatili ambavyo wamekuwa wakifanyiwa kwenye jamii ili vipatiwe ufumbuzi wa haraka.

# Mlengwa TASAF aupa kisogo umaskini

**Na Marco Maduhu,** ITILIMA

MLENGWA wa mpango wa kunusuru kaya maskini katika kijiji cha Nanga, Itilima mkoani Simiyu, Mayeye Sahani, ameondokana na umaskini baada ya kupata manufaa kutokana na miradi aliyoiendesha kupitia ruzuku aliyopewa.

Kutokana na hali hiyo, amejiondoa katika mpango huo unaotekelezwa na Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF).

Sahani alibainisha hayo juzi wakati maofisa wa TASAF kutoka makao makuu walipotembelea kwenye kijiji hicho, ili kuona maendeleo ya walengwa wa mpango huo, walivyozitumie fedha za TASAF kujikwamua kiuchumi.

Alisema kwa sasa amejitoa kwenye mpango huo baada ya kuinuka kiuchumi na si maskini tena. Kwa sasa anamiliki duka kubwa kijijini hapo pamoja na mashamba na kwamba ameamua kuachia kaya nyingine ambayo ni maskini iingizwe TASAF.

"Mimi kwa sasa siyo maskini tena bali ni tajiri sababu maisha yangu ni mazuri. Nina duka kubwa kama mnavyoliona. Pia nina mashamba nalima pamba, hivyo sioni haja ya kuendelea kuwa TASAF nimejitoa," alisema Sahani.

"Mali zangu hizi nimezipata kupitia pesa ya TASAF. Mara ya kwanza kupokea mwaka 2015, nilikodi shamba nikalima bustani ya mboga na nyanya. Baada ya hapo nikaanza kulima pamba ndio imenitoa kwenye umaskini hadi kumiliki duka kubwa hapa kijijini," aliongeza.

Mlengwa mwingine, Ruli Ng'habi, mkazi wa kijiji hicho, alisema yuko mbioni kujitoa kwenye mpango huo kwa kuwa sasa ana kondoo tisa, mbuzi wanne, nyumba mbili alizowekeza mabati na anajenga pia nyumba nyingine ambayo iko kwenye hatua ya upauaji.

Ofisa Ufuatiliaji wa TASAF katika Halmashauri ya Wilaya ya Itilima, Paulo Tibabilila, alisema wana walengwa 5,823 ambao hali zao za kiuchumi ni nzuri na kutoa wito kwao waendelee kuwekeza pesa hizo kwenye uzalishaji ili ziwakwamue kiuchumi.




Mkurugenzi Mkuu wa Tume ya Sayansi na Teknolojia (COSTECH), Dk. Amos Nungu (katikati), akikata utepe kuzindua vitabu vya mradi wa kuwajengea uwezo wanafunzi wa shule za sekondari wanaosoma masomo ya sayansi na Fizikia, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Sababu viongozi kushindwa kuongoza ushirika zatajwa

**Na Mohab Dominick,** KAHAMA

VIONGOZI wengi wa vyama vya ushirika wanakwama kuongoza sekta hiyo muhimu kutokana na wengi wao kutopata mafunzo elekezi, imeelezwa.

Pia viongozi hao wanapoaminiwa kuongoza ushirika, hawana budi kujengewa uwezo kwa kuwa ndiyo chachu kuongoza kwa kufuata maadili na uadilifu mkubwa huku wakijali maslahi makubwa ya wanachama.

Kaimu Mrajisi Msaidizi wa Vyama vya Ushirika anayesimamia Sheria na Usajili kutoka Ofisi ya Mrajisi Makao makuu Dodoma, Grace Mwangende, alisema hayo juzi katika Mkutano Mkuu Maalumu wa Chama cha Ushirika Wilaya ya Kahama (KACU) ulioambana na uchaguzi wa viongozi wa bodi ya chama hicho.

Mwangende alisema baada ya uchaguzi mkuu wa KACU kufanyika, ni lazima viongozi wapate mafunzo ya uongozi mahali popote watakapokuwa wamechagua iwe Shinyanga au Kahama ili kuwajengea uwezo wa kuongoza.

Mwangende ambaye katika uchaguzi huo alikuwa Mwenyekiti wa Kamati ya Uchaguzi, alisema kama viongozi watapata mafunzo, kuna uwezekano mkubwa wa kupungua malalamiko kutoka kwa wanachama hali ambayo itakuwa rahisi kukiongoza chama kwa kuwa watakuwa na upeo wa uongozi.

Naye Mrajis Msaidizi wa Ushirika Mkoa wa Shinyanga, Hilda Boniphace, aliwataka viongozi waliochaguliwa, wasitumie makundi ya nje katika kuharibu ushirika na kuwataka wajumbe wapya wa bodi kuja na mawazo chanya.

Alisema wawakilishi wao ambao ni wanachama wanategemea uongozi huo kufanya kazi kwa asilimia 100 huku akiutaka uongozi wa bodi kutunza mambo yao ya ndani na kuongeza kuwa tabia ya kutoa siri husababisha migogoro katika vyama vingi vya ushirika.

Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga, Zainab Telack, aliyekuwa mgeni rasmi katika uchaguzi huo, alisema chama hicho cha ushirika kimeupa sifa mkoa na nchi kwa ujumla kwa kusimamia vizuri mambo yake kuliko vyama vingine.

Alisema wajumbe katika uchaguzi huo wanatakiwa kuangalia maslahi ya ushirika katika kuchagua viongozi na kuongeza kuwa chama hicho kwa sasa kinatarajia kuanzisha kiwanda cha mafuta ya kula na kuongeza kuwa: "Kwa sasa hatutaki kuchagua viongozi ambao wataenda kuwa mchwa katika chama."

Miongoni mwa walioshinda katika uchaguzi huo ni Mwenyekiti wa Bodi, Emmanuel Charahani na Geoffrey Mbutu ambaye anakuwa makamu wake ambao hawakuwa na wapinzani. Walichaguliwa kwa mara ya pili kuongoza chama hicho.



# RC ataka tathmini ya mafuriko

**Na Augusta Njoji,**
DODOMA

MKUU wa Mkoa wa Dodoma, Dk. Binilith Mahenge, ameagiza wataalamu wa Halmashauri ya Jiji la Dodoma kwa kushirikiana na wananchi, kufanya tathmini ya nyumba zilizokumbwa na mafuriko katika Kata ya Nkuhungu ili kutoa suluhisho la kudumu la tatizo hilo.

Pia amepiga marufuku wananchi kurudi kwenye makazi yao kwenye mitaa ya Mnyakongo, Bochela, Mtubi na Salama kutokana na kukumbwa na mafuriko mara kwa mara.

Akizungumza juzi na wananchi baada ya kujionea nyumba zikiwa zimezingirwa na maji huku wengine wakikimbia makazi yao, Dk. Mahenge alisema tathmini ya nyumba hizo ifanyike katika makundi mawili ya wenye vibali halali na waliojenga kwa kuvamia.

Dk. Mahenge aliwataka wananchi kuwasikiliza viongozi na kuacha kung'ang'ania kukaa mabondeni ili kujiepusha na adha ya mafuriko msimu huu wa mvua.

"Katika taarifa yenu mmeniambia kuna watu humu walipimiwa na iliyokuwa CDA (Mamlaka ya Ustawishaji Makao Makuu) na wengine wamevamia na kutokana na mvua zilizonyesha, maji yamevuka eneo lake na kuingia kwenye makazi ya watu. Nataka mkurugenzi ufanye tathmini nyumba ngapi zimepata madhara na ni watu wangapi wanahitaji msaada," alisema.

Pia alisema kuna watu kwa jitihada za Mbunge wa Dodoma Mjini, Anthony Mavunde, wamehifadhiwa na anawalipia kodi.

"Nataka nipate idadi na watu hao wanahitaji msaada kiasi gani. Tunaweza kuongea na watu wa Red Cross (Chama cha Msalaba Mwekundu) tukapata maturubai watu hawa wakawa salama," alisema.

Pamoja na hayo, Mkuu huyo aliagiza mamlaka husika kutengeneza kikosi kazi cha kuangalia namna ya kuondoa, kupunguza au kudhibiti maji hayo yasiendelee kuongezeka katika eneo hilo.

Alisema Jiji la Dodoma limezindua mpango kazi wa ardhi yote ya Jiji hilo wa mwaka 2019 hadi 2039 na kuwataka wananchi waepuke kununua maeneo bila kupitia Jiji au kujenga nyumba bila kuwa na kibali.

Naye Mkurugenzi wa Jiji la Dodoma, Joseph Mafuru, alisema historia inaonyesha mwaka 1985 pembezoni mwa eneo hilo kulipimwa viwanja na eneo dogo likabaki kuwa eneo la maji lakini baadhi ya watu wakaingia na kujenga pembezoni na miaka miwili ya karibuni na kusababisha maji ya mvua kuingia katika makazi ya watu.

"Mara kadhaa tumejaribu kuondoa maji, lakini tathmini inaonyesha ukiondoa maji yanakwenda kuleta athari katika maeneo mengine yaliyo salama hivyo tupo kwenye mchakato wa kufanya tathmini ya idadi ya watu ili watafutiwe eneo salama kwa makazi," alisema.

Kwa upande wake, Mavunde aliomba ifanyike haraka tathmini ili wananchi hao wapate makazi mbadala.



Waandishi wa habari wa jijini Dodoma, wakitoka kwenye gari baada ya kukwama kwenye maji yaliyojaa katika korongo, lililopo Mtaa wa Ndachi, Kata ya Mnadani jana na kusababisha watu kushindwa kupita kutokana na mvua kubwa zinazoendelea kunyesha. **PICHA: PETER MKWAVILA**

# SIDO yasisitiza uzalishaji endelevu

**Na Renatha Msungu,**
DODOMA

SHIRIKA la Kuhudumia Viwanda Vidogo (SIDO) Mkoa wa Dodoma, limewataka wajasiriamali kuwa na uzalishaji endelevu badala ya kusubiri kuishiwa bidhaa sokoni.

Ofisa Ufundi wa Shirika hilo, Nyangusi Mollel, aliyasema alipokuwa akihitimisha mafunzo ya usindikaji wa vyakula yaliyoandaliwa na SIDO kwa kushirikiana na Mamlaka ya Elimu Tanzania (TEA).

Alisema ili kudumu kwenye soko la biashara inatakiwa kuwapo na uendelevu wa uzalishaji wa bidhaa ili kukidhi mahitaji ya soko.

"Kwenye uzalishaji wa bidhaa angalia soko linahitaji nini pia jifunze kutoka kwa wenzako wana nini cha peke yako kuhusu wewe," alisema.

Alisema shirika hilo limekuwa likitoa mafunzo mbalimbali ya usindikaji wa vyakula , utengenezaji wa bidhaa za ngozi, utengenezaji sabuni,

mafuta na bidhaa mbalimbali.

Aliwataka wananchi kuchangamkia fursa za kupata mafunzo ili kuboresha biashara na kupata mbinu za kufikia masoko ya ndani na nje ya nchi.

"Jiwekee pia mpango kazi na uwe makini nao na ujue bidhaa zako unapeleka kwenye soko gani, mpango unatakiwa ukuvute wewe na unatakiwa uwe msimamizi wa kazi zako," alisema.

Naye Ofisa Miradi wa SIDO Mkoa wa Dodoma, Stephano Ndunguru, aliwataka wajasiriamali kuwa na utaratibu wa kutafuta taarifa mpya.

Mmoja wa washiriki wa mafunzo hayo, Isack Mota, aliwataka wajasiriamali kuungana ili kufanya kazi kwa pamoja.

"Wajasiriamali tuungane ili kufanya kazi kwa pamoja ukiwa peke yako ni vigumu kupata misaada au mikopo kutoka taasisi za serikali au binafsi," alisema.

Alisema wakati huu Jiji la Dodoma lina watu wengi kutokana na ujio wa serikali ni muhimu kujipanga kuzalisha bidhaa nyingi zenye ubora ili kuchangamkia fursa ya kuuza bidhaa kwa wingi.

Mota alisema bidhaa zinapokuwa na ubora zinamhakikishia mjasiriamali soko la uhakika.

# TAKUKURU yadhamiria kukabili rushwa ya ngono

**Na Renatha Msungu, DODOMA**

TAASISI ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) imesema kwa miaka mitano ijayo imejipanga kupambana na rushwa ya ngono ambayo hivi sasa imeshamiri katika sekta mbalimbali hasa elimu.

Sambamba na hilo, imedhamiria kuboresha mifumo ya kiutendaji ili kudhibiti mianya ya rushwa kwenye maeneo mbalimbali nchini.

Mkurugenzi Mkuu wa taasisi hiyo, Brigedia Jenerali John Mbungo, alsiema hayo juzi kwenye mkutano mkuu wa

mwaka wa kutathmini utendaji kazi wa taasisi hiyo kuanzia Julai, 2019 hadi Juni, mwaka jana jijini hapa.

Alisema lengo la kufanya hivyo ni kutaka Tanzania iendelee kushika nafasi za juu kimataifa katika suala la udhibiti wa rushwa.

Aidha, alisema wamejipanga kuhakikisha wanamalizarushwa ya ngono ambalo lilikuwa limeshamiri katika kipindi cha nyuma hasa katika taasisi za elimu na kazini ambapo watu wanakosa haki zao hadiwatoe rushwa.

"Ili kuendelea kushika nafasi za juu kimataifa

katika mapambano ya rushwa lazima jitihada ziwepo ikiwamo kuendelea kushirikiana na jamii ili taifa lizidi kupanda nafasi za juu kwenye utafiti wa kimataifa unaofanywa na Taasisi ya Kimataifa ya

Utafiti wa masuala ya Rushwa Transparency International (TI)," alisema.

Alisema katika viwango vilivyotolewa hivi karibuni na taasisi hiyo, Tanzania ilishika nafasi ya 94 katika nchi 180 zilizofanyiwa utafiti duniani baada ya kupata alama 38.

Alisema jitihada zao zitaendelea katika mapambano ya rushwa sehemu zote ili kuhakikisha wanapanda Kimataifa.

"Hii miaka mitano tumepanga kuchukua hatua zifuatazo ili kudhibiti vitendo vya rushwa, ni kuimarisha mifumo ya utendaji kazi, kudhibiti matumizi mabaya ya fedha za umma, kubuni na kutekeleza mikakati mipya ya kupambana na rushwa," alisema.

Alibainisha pia kuhamasisha na kushirikisha jamii katika mapambano ya rushwa, kutoa elimu na kuendelea kufanya utafiti katika maeneo mbalimbali.

Mkurugenzi Mkuu huyo alisema pamoja na kuboresha mifumo, watahakikisha kila mwananchi anapata haki yake bila kuonewa.

Naye Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Dk. Binilitih Mahenge, alipongeza TAKUKURU kwa kufanikiwa kudhibiti vitendo vya rushwa hapa nchini.

Alisema ili kujenga nchi iliyoendelea ni lazima kupambana na rushwa ambayo ndio adui mkubwa wa maendeleo.



# Maradhi yatajwa kikwazo biashara kwa wanawake Z'bar

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MTAALAMU wa masuala ya maendeleo ya biashara, Yahya Khatibu Haji, amesema maradhi ya corona yamewaweka wanawake wa Zanzibar katika hali mbaya ya kiuchumi hasa kwa kuwa kundi kubwa la wanawake wanajishughulisha na biashara na ujasiriamali.

Aliyasema hayo jana katika kongamano la maadhimisho ya Siku ya Wanawake Duniani wakati akiwasilisha mada kuhusu biashara, lililofanyika Maisara mjini Unguja. Kongamano hilo liliandaliwa na Chama cha Waandishi wa Habari Wanawake Tanzania (TAMWA) Zanzibar.

Alisema bado wajasiriamali wa Zanzibar wanashindwa kutumia vyema maendeleo ya sayansi ya teknolojia jambo ambalo kwa sasa linachukua umuhimu wa pekee katika kufikia masoko.

"Kwa kweli ipo haja ya kuangalia namna ya kupata wateja na kufikia masoko kama hujui kutumia mitandao ni wazi kuwa watabaki nyuma kundi ambalo ni wanawake," alisema. Akichangia mada katika kongamano hilo, Faida Mohamed Shaibu, ambaye ni mjasiriamali wa bidhaa za kusindika, alisema tatizo kubwa linalowakabili ni soko, ushuru mkubwa, ukosefu wa vifungashio unasababisha changamoto mbalimbali za kufika mbali.

Alisema vifungashio kwa ajili ya bidhaa zao vikiwamo vya kuhifadhia sabuni za maji, upatikanaji wake Zanzibar ni wa shida jambo ambalo linawarudisha nyuma kibiashara.

Pia alisema kwa upande wa soko ni gumu kutokana nab ado jamii kuthamini zaidi vitu kutoka nje ya nchi kuliko vinavyozalishwa nchini.

Naye Makamu Mkuu wa Chuo Kikuu cha Taifa Zanzibar (SUZA), Dk. Zakia Mohamed, alisema wakati umefika sasa kwa wanawake kujitoa zaidi katika kufikia maendeleo.

Aliwataka wanawake waliopewa nafasi za uongozi kuzitumia vyema ikiwa ni pamoja na kujua shida za watendaji wa chini ili kufikia maendeleo ya taasisi. "Uongozi ni dhima kubwa katika kufikia maendeleo ya dhati, ili kwenda sambamba na maendeleo hayo hakuna budi kuona kuwa wanatatua changamaoto kwa wanaowaongoza," alisema.

Akifungua kongamano hilo, Mkurugenzi wa TAMWA Zanzibar, Dk. Mzuri Issa Ally, alisema uwapo wa takwimu sahihi za kiuchumi kwa wanawake kutasaidia kukuza ustawi wa wanawake na kuweka mipango mizuri ya maendeleo visiwani Zanzibar.

Alisema hadi sasa Zanzibar hakuna takwimu sahihi za kiuchumi ambazo zinaonyesha kipato cha mwanamke hali ambayo inapelekea kutojua uhalisia wa ongezeko la pato kwa jamii hususani wanawake kwa kuwa takwimu hizo hujumlishwa kwa watu wote na hakuna mgawanyo wa jinsia.



Aliyekuwa Kaimu Waziri wa Afya, Ustawi wa Jamii, Wazee, Jinsia na Watoto Zanzibar, Simai Mohamed Said (kushoto), akikabidhi ofisi kwa waziri mteule wa wizara hiyo, Nassor Ahmed Mazrui, jijini Zanzibar jana, baada ya kuapishwa na Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk. Hussein Mwinyi, juzi. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Mwinyi ataka tija katika kilimo

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

RAIS wa Zanzibar, Dk. Hussein Mwinyi, ameitaka Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo kuimarisha sekta ya kilimo kwa kukifanya kuwa cha kibiashara ili kilete tija.

Dk. Mwinyi aliyasema hayo juzi, Ikulu jijini Zanzibar, alipokutana na uongozi wa wizara hiyo, ikiwa ni mkutano kwa ajili ya kuripoti utekelezaji wa maagizo aliyoyatoa kwa mawaziri na makatibu wakuu alipowaapisha.

Alisema wizara hiyo ihakikishe kilimo kinaendelezwa na kuwa cha kibiashara hatua ambayo itawasaidia wakulima wadogo ambao watanufaika na sekta hiyo tofauti na ilivyo sasa.

Kilimo kinachofanyika hivi sasa, alisema bado hakijawa na faida kwa wakulima na hata Serikali ya Zanzibar na lile lengo lililokusudiwa la kuhakikisha chakula cha kutosha hasa mchele unazalishwa Zanzibar halijafikiwa.

Kuhusu ufugaji, Dk. Mwinyi alisema bado ni tatizo kwa sababu wafugaji wajawasaidia, hivyo ni vyema kukatafutwa wafugaji wakubwa kuendesha shughuli hizo na hatimaye kuwasaidia wafugaji wadogo wadogo. Alieleza azma yake ya kutaka mabadiliko katika sekta ya kilimo na sekta hiyo iondoke hapo ilipo na kuwa na tija na mafanikio makubwa.

Dk. Mwinyi alisisitiza umuhimu wa kuweka utaratibu maalum wa kutafuta wawekezaji wa kilimo kwa kupitia Mamlaka ya Uwekezaji Zanzibar (ZIPA) na kuweka mazingira mazuri kwa wawekezaji wa ufugaji.

Rais Dk. aliitaka wizara hiyo ya kuhakikisha inazalisha zaidi badala ya kutoa huduma kama ilivyo hivi sasa.

Naye Katibu Mkuu wa Wizara hiyo, Mariam Juma Abdalla, alisema lengo kuu la wizara hiyo ni kufanya mageuzi katika sekta ya kilimo kuwa cha kisasa, jumuishi na chenye ushindani ambacho kitachangia sekta ya viwanda na utalii ili kuleta tija na maisha bora kwa wananchi.

Pia alisema sekta ya kilimo inatoa ajira rasmi kwa wastani wa asilimia 40 na zaidi ya asilimia 70 ya wananchi wanategemea sekta hiyo kwa njia mbalimbali katika kujipatia kipato na kuimarisha maisha yao.

Wizara hiyo, alisema imechukua hatua mbalimbali za kuanzisha uhusiano kwa kuwapatia wakulima na wafugaji mikopo nafuu kupitia Benki ya Maendeleo ya Kilimo ya Tanzania (TADB), benki ya PBZ na CRDB.

Alisema wizara inaendelea kupambana na wadudu waharibifu wa matunda kwa kusambaza mitego ya kunasa wadudu hao pamoja na kutoa taaluma kwa wakulima katika kukabiliana na wadudu waharibifu na maradhi ya kupitia halmashauri

Mariam alisema wizara inaendelea kushirikiana na Wizara ya Ardhi kuyatambua, kuyapima na kuyapatia hati miliki maeneo ya kilimo.

# Othman awataka Wazanzibari wamuunge mkono Rais

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MAKAMU wa Kwanza wa Rais wa Zanzibar, Othman Masoud Othman, amewataka Wazanzibari kumuunga mkono Rais katika juhudi za kuleta maendeleo ili kufanikiwa kwa urahisi.

Aliyasema hayo jana huko Msikiti wa Mwembe Tanga Mjini Unguja wakati alipohudhuria hitima ya kumwombea dua aliyekuwa Makamu wa Kwanza wa Rais, Maalim Seif Sharif Hamad, aliyefariki dunia mwezi uliopita.

Alisema katika kipindi hiki Zanzibar imepata fursa ya kuwa na kiongozi mzuri mwenye maono, hivyo hakuna budi kumuunga mkono ili kufikia malengo yaliyokusudiwa.

"Tumuunge mkono Rais na serikali ili iwe rahisi kutatuliwa shida zetu mbali mbali" alisema Othman.

Alisema hayo yote hayatafikiwa kama Wazanzibari hawatakuwa kitu kimoja na kuwaomba waendeleze umoja wa kitaifa uliopo.

Makamu huyo wa Rais alisema endapo Wazanzibari watauvunja umoja huo, ni sawa na kumdhulumu Maalim Seif ambaye alikuwa muumini mkubwa wa umoja wa kitaifa.

"Wazanzibar wenzangu dua nyingine kubwa ya kumwombea kiongozi wetu ni kuendeleza yale aliyotuachia ambayo umoja wa Wazanzibari," alisema.

Aliwataka kuendeleza upendo ambao umeleta amani nchini bila kujali vyama vya siasa, dini na rangi.

"Kila mtu ni shahidi kwa yale maisha na khulka za Mzee wetu na matendo yake kwa jamii yetu ndani na nje," alisema.

Alisema mikusanyiko ya dua ni dalili kuwa kiongozi huyo alikuwa na mapenzi makubwa ya watu hivyo hakuna kubudi kuenziwa na kukumbukwa kila wakati.

"Ni wajibu wetu kusimamia ya kuyaendeleza, mimi nimepewa moja ya dhamana ya kuyaendeleza yale aliotuachia Maalim Seif nawahakikishia kwa uwezo wake Allah sitowaangusha," alisema.

Hata hivyo, alisema hajapitia machungu aliyoyapata Maalim Seif katika siasa lakini alikubali kupokea kijiti hicho si kuwa wengine hawapo.

Naye Makamu Mwenyekiti wa ACT – Wazalendo, Juma Duni Haji, alisema Maalim Seif alikuwa akiwapenda Wazanzibari kama alivyokuwa akiwapenda watoto wake. Alisema licha ya kupata changamoto nyingi wakati uchaguzi, hakuacha mapenzi yake kwa wananchi wake.

Alisema katika kuelekea nani awe mrthi wake, kamati ya uongozi ya chama hicho ilibebwa na hekima na busara ili umoja uliopo usije ukatetereka.



**JUX**
UKURASA 13

Nipashe
MWANGA WA JAMII
BT
BURUDANI TELE
JUMAMOSI MACHI 6, 2021



# JASINTA MAKWABE

## Achukizwa wanamuziki wasiojua kuimba

MWANAMITINDO na mpambaji wa video za muziki kutoka Tanzania, Jasinta Makwabe, amesema waliotoka katika fani hiyo na kukimbilia katika muziki wengi wao hawajui kuimba.

Akizungumza hivi karibuni, Jansita amesema hakuna hata mmoja ambaye alikuwa video Queen ameweza kuvutia mashabiki kutokana na uimbaji mzuri, badala yake wametawaliwa na tamaa ya pesa.

Baadhi ya warembo ambao walikuwa wakipamba video za wanamuziki na sasa wamegeuka waimbaji ni Gigy Money, Lulu Diva na Amber Lulu.

"Waliotoka katika kazi ya kupamba muziki na kukimbilia muziki wengi wao wametawaliwa na tamaa tu, lakini hawajui kuimba," amesema Jasinta.

Ameeleza yeye ataendelea katika kazi yake hiyo ambayo imemkuza jina na sasa anafanya kazi na wasanii wakubwa Afrika Mashariki.

Aidha, ameelezea ndoto zake kwa sasa ni kufanya video na wanamuziki wa Marekani Chris Brown na Wizkid na Burna boy kutoka Nigeria.

Hata hivyo amewataka wanaofanya kazi ya video kuacha kutumika kama sabuni, badala yake wajiamini na kuthaminisha kazi zao.

"Nawaomba sana wafanye kazi kwa maslahi, badala ya kutumika na kutupwa pale kazi inapomalizika, muhimu wajiamini kwani wao wanafanya kazi kubwa kupamba video hadi watu wanapenda," amesema.

BASI SAWA

## Country kwani wenyewe hawawezi kusema?

RAPA Country Wizzy kutoka lebo ya Konde Gang`, amesema ukimya wa wasanii wenzake, Killy na Cheed, unatokana kuwa katika maandalizi ya kazi yao kubwa itakayotambulishwa hivi karubuni.

Wasanii hao ambao wapo katika lebo hiyo, wapo kimya tangu watoke katika lebo ya Kings Music ya Alikiba.

"Ukimya wa Killy na Cheed unasababishwa na ubize wa kutengeneza Album, ambapo walipanga watoke na style hiyo na wapo katika hatua ya mwisho kukamilisha Album yao na kabla ya mwezi wa tano itakuwa tayari, Killy ana ngoma moja kali sana kwenye Album yake ninayo kwenye simu yangu". Amesema




## Nandy waambie waache umbea

MWANAMUZIKI wa kike anayetingisha kwa sasa, Nandy, amewataka watu kuacha kumuuliza kuhusu madai ya kuwa na ugonjwa wa UKIMWI, akisema suala hilo sawa na unyanyapaa.

Akizungumza kupitia Insta Stori, amesema maswali hayo yatawavunja moyo wagonjwa ambao watahisi wao si bidadamu kama wengine.

"Swali la UKIMWI pia muache kuniuliza, labda unataka nikupunguzie kidogo na tuheshimiane, mnafanya hata wale wanaoumwa kweli wajione sio binaadam wa kawaida hofu ya Mungu itawale" amesema Nandy.





## Muumin angaika tu utampata Chamilione

KIONGOZI wa kundi la Special Band linalopiga muziki wa dansi, Mwinjuma Muumin, amesema anatamani kumshirikisha msaani wa Uganda Jose Chamilione, katika moja ya nyimbo za bendi yake.

Amesema, bendi hiyo kwa sasa imerekodi nyimbo mpya kama 'Fenesi, Yatima Mzee na Mwanangu. Pia wanajiandaa kurekodi nyingine Kwa Mpangarange Sihami, Vumbi la Congo na Jibwa la Kizungu'.

"Ninatamani wimbo wa mwisho wa albamu yetu ya kwanza nimshirikishe msanii wa muziki wa kizazi kipya kama Jose Chamlione wa Uganda kama itawezekana ili aweke vionjo vyake," amsema Muumin.

## Nani Mtemi? Wanagombania ndizi, mgomba si wao

**Na Adam Fungamwago**

WASWAHILI wana utajiri wa methali. Kuna hii inayosema 'wanagombania ndizi na mgomba si wao.' Maana ya methali hii ni kwamba kuna watu wana tabia ya kugombania, au kupenda vitu ambavyo siyo vyao, au hawana uwezo wa kuvipata.

Leo tunajikita kwenye filamu iitwayo 'Nani Mtemi' Ni filamu inayoonyesha jinsi gani, watu wanaweza kuzozana, kufanyiana ubaya na kutishiana amani kwa kitu ambacho wala si chao, na wala hawana uwezo wa kukipata.

Imechezwa na Mohamed Fungafunga, maarufu kama mzee Jengua wakati wa uhai wake, mzee Msisiri, Odobe Okoye, Sara Obby, Robby Katugulu, Genovera Innocent na wengine wengi.

Inaanza kwa kuonyesha vijana wawili kijijini hapo, Muki na Kilesa wakimpenda msichana mmoja, anaitwa Nusra. Siyo kwamba kulikuwa hakuna wanawake wengine kijijini hapo, bali vijana hao walimpenda kwa sababu nadhani alikuwa mrembo zaidi kuliko wengine.

Muki ni mtoto wa mzee Jengua ambaye kijijini hapo anasifika kwa ukali na ubabe wake, huku Kilesa yeye akiwa ni mtoto wa mzee Msisiri ambaye ananuka kwa uchawi.

Keshehe inaanza kwa vijana hao kuweka nia ya kutaka kumuoa msichana huyo mbele ya wazazi wao.

Sasa kila mmoja akamhakikisha kijana wake kuwa ni lazima amuoe Nusra.

Kivumbi kilianza pale mzee Jengua alipomkuta mtoto wa Msisiri Kilesa akiwa amesimama na binti huyo. Povu lilimtoka na kutishia kuwakatakata vipande wote wawili na watu wasijue ipi nyama ya mwanaume au ya mwanamke.



Siku nyingine nayo, mzee Msisiri alimfuma Nusra akiwa amesimama na mtoto wa mzee Jengua, ambaye ni Maki. Yeye akatishia kuwageuza paka au nyoka wote wawili.

Kijiji kikageuka kuwa cha ugomvi. Mzee Msisiri akaenda nyumbani kwa mama Nasra kupiga mkwara kuwa binti asipomkubali kijana wake, atawaua wote. Jengua naye akaenda nyumbani hapo kwa wakati wake na kutishia kuwaua kwa shoka.

Ili mradi tu Nusra na mama yake hawakukaa kwa amani. Wenyewe kwa wenyewe nao mzee Jengua na Msisiri walipokutana walipigana mkwara wa kufa mtu.


Mama Nasri aliwaambia wote kuwa binti yake hatoolewa na kijana yoyote kijini hapo.

Maki na Kilesa nao wakikutana njiani ni bifu tu moja kwa moja, ili mradi tu ikawa tafrani moja kwa moja.

Siku moja isiyo na jina, hali ilipozidi kuwa mbaya, kila upande ukiona kuwa huenda haukubaliwi kwa sababu upande mwingine unataka kukubaliwa, kila mzee alitoka na mtoto wake kwenda kufanya varangati nyumbani kwa kina Nusra.

Walipofika walimkuta kijana mmoja mgeni aliyekuwa tofauti na wao. Alikuwa ametoka mjini. Kijana huyu alijitambulisha kama mwanajeshi aliyetoka Dar na yeye ndiye mchumba wa Nusra tangu zamani. Wote wakanywea.





## Jux acha kuwatania watu

MSANII wa muziki wa miondoko ya R&B nchini, Juma Jux, ameanza kuleta nyodo, baada ya kueleza mjengo wake mpya ambao umetikisa mitandaoni, kuwa eti bado haujafikia ndoto yake.

Amsema kutokana na kuwa na tabia ya kupenda vitu vizuri, nyumba yake hiyo anaona bado hajafikia nyumba ambayo anataka amiliki.

"Ile bado sio nyumba ya ndoto yangu na ambayo nataka kuishi japo tunajaribu tu kidogo na Mungu katujaalia, pale nakaa ndiyo lakini sio nyumba ya ndoto yangu mimi napenda sana nyumba na vitu vizuri, bado naendelea kupambana ili kufikia nyumba ambayo nataka niwe nayo" amesema Jux

## KOLABO 5 BONGO 2021

**Na Adam Fungamwango**

MSANII wa muziki wa kizazi kipya, Nandy, ametoa ngoma moja kali iitwayo 'Leo Leo', akimshirikisha gwiji wa muziki wa sokous na rhumba Afrika, Mkongomani Koffi Olomide.

Ni ngoma ambayo imeanza kusumbua kwenye vyombo vya habari, kama vile redio, televisheni, pamoja na mitandao ya kijamii.

Ni ngoma ambayo ina maneno ya mapenzi, lakini kikubwa zaidi ni jinsi Koffi alivyoubadilisha muziki huo na kuonekana ni wa dansi zaidi kuliko bongo fleva, lakini ikiwa kwenye mwelekeo wa kibongo fleva pia.

Imetoka Februari 26, lakini kwa siku hizi chache tu, imeshatazamwa na watu milioni moja na ushehe hivi.

Wakati ngoma hiyo ikinyanyasa, tunawakumbusha tu kuwa wasanii wa Kitanzania kwa sasa wamekuwa wakijichanganya na kutafuta wasanii wenzao wa hapa ndani, au wa nje, ili kuunganisha vipaji vya na kutoa ladha tofauti ya upigaji na uimbaji, lakini pamoja na maudhui.

Wenyewe wanaita kolabo. Leo tunawaletea baadhi ya kolabo zilizofanya vema sana kama hii ya Nandy na Koffi.

**Stamina Ft Profesa Jay-Baba**

Ni bonge la kolabo ambalo lilimfanya hata Rais Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dk. John Magufuli kuomba apigiwe alipokwenda kufungua kituo kimoja ya habari nchini.

Mwenyewe alikiri hadharani kuwa ni moja kati ya nyimbo ambazo anazihusudu mno kutokana na kuwa na ujumbe mzuri kwa jamii na mafundisho.

Unamhusu kijana mmoja anayemzodoa baba yake eti kutokana tu na umasikini wake, akimsimanga kuwa mbona wazee wenzake ni matajiri, lakini yeye ni masikini wa kutupwa.

Baba akamjibu majibu ambayo hakurudia tena kuulizwa maswali ya kipuuzi kama yale.

Kwanza alimwambia hakuwa mtoto wake wa damu. DNA ilikataa. Lakini alimsomesha, akakimbia shule, sasa akamuuliza kosa lake hapo liko wapi?

Ni moja kati ya kolabo bora zaidi nchini kati ya Stamina akimshirikisha Profesa Jay.

**Diamond Platinumz ft Koffi Olomode-Waah**

Diamond, ndiye aliyekuwa wa kwanza kumleta Koffi Olomide nchini Tanzania na wanatengeneza bonge la kolabo moja, wakatoa ngoma iliyoitwa 'Waah'.

Kama kawaida ya Koffi. Alibadilisha midundo hiyo kuwa ya dansi na kuufanya wimbo kuchezeka.

Hata hivyo, asilimia kubwa ya wimbo huo unatokana na wimbo wa Koffi ambao ulitokea kupendwa sana nchini na kupigwa kwenye sherehe mbalimbali za harusi na matamasha, 'Papa Mobimba'.

**Roma ft Stamina (Rostam)-Kaka Tuchati**

Wakali hawa wawili ambao mara nyingi wana tabia ya kuungana na kutoa ngoma, walifanya hivyo tena kwenye ngoma iliyoondokea kupendwa mno 'Kaka Tuchati.'

Ni ngoma ambayo ilitungwa wakati Tanzania na Dunia kwa ujumla ikiwa kwenye janga la magonjwa ya kupumua, mwanzoni kabisa mwa mwaka 2000, ikielezea jinsi gani ya kujikinga.

Ilikuwa ni moja kati ya kolabo iliyotoa ngoma bora nchini Tanzania.

**Nandy Ft Ali Kiba-Nibakishie**

Nandy hajambo kwa kolabo. Kuna wakati alimtafuta Ali Kiba na kufanya kolabo moja kali, wakitoa ngoma moja walioiita 'Nibakishie'

Ngoma hii ilikubalika na haikushangaza kuwa ni moja kati ya kolabo 10 bora ya mwaka 2000.

**Rayvanny Ft Zuchu-Number One**

Rayvanny yeye aliamua kufanya kolabo na msanii Zuchu kwenye ngoma yake aliyoiita 'Number One.'

Ni wimbo wa mapenzi, ambapo wapenzi wameonekana kuonyesha hisia zao, kila mmoja akionyesha jinsi anavyomthamini mwenzake.

Ngoma hii ilipendwa na kuwafanya wasanii hao kuingia kwenye orodha ya kufanya kolabo bora nchini.






# TI, mkewe wa kana ubakaji

RAPA Mmarekani T.I. na mkewe,Tiny Harris, wamekanusha madai ya ubakaji, utekaji nyara na uuzaji dawa za kulevya.

Kulingana na mtandao wa PageSix, wakili wa wanandoa hao amesema wanakanusha kuwa madai hayo hayajathibitishwa.

Kauli hii ilikuja baada ya wakili, Tyrone A. Blackburn kuomba kufanyike uchunguzi wa makosa ya jinai dhidi ya wenzi hao baada ya wanawake kadhaa kujitokeza wakiwakilalamika kuwa walitekwa na kupewa dawa za kulevya kwa nguvu.



## Duh! mkwara wa mama mkwe hatari

MTANGAZAJI wa vipindi vya burudani nchini Nigeria, Afia Schwarzenegger , ametoa mkwara kuwa watoto wake wa kiume kutokuwa na uhusiano wa kimapenzi na wasichana waliosoma Ghana,

Akizungumza baada ya picha ya mtoto wake mmoja akiwa na rafiki yake wa kike, Afia amesema wanawe ambao ni mapacha ni uwekezaji wake na hatawaruhusu kuoa msichana yeyote anayepata masomo yake nchini humo.


Amesema James na John Ian Geiling Heerdegan kwa sasa wako shuleni kusoma na hawana nafasi ya wasichana na kuvionya vyombo vya habari kuacha kuwataja marafiki wa kike wa mapacha wake kama wakwe zake.

## Tyrese aimba wimbo kujiliwaza

MWANAMUZIKI wa Marekani, Tyrese Gibson, amejaribu kusahau yaliyopita tangu aachane na mke wake baada ya kutoa singo inayozungumzia maisha yake ya ndoa.

Kupitia ukurasa wake wa Instagram taa huyo wa muziki, amesema anajaribu kuanza ukurasa mpya kukutana na watu wapya.

"Samahani kwa dhambi zangu na samahani kwa chochote nilichowahi kumtendea mtu yeyote badala yake ninajua au la tu natumahi kuwa umeipata katika moyo wa kunisamehe ..... bado sijakutana na mtu wangu BORA na ninajua, "ameandika.





## Toke akubali umbo la kutengenezwa

MWANAMITINDO wa Nigeria, Toke Makinwa. Amesema wanaume hawachangii wanawake kufanya upasuaji wa kurekebisha viungo, badala yake ni utashi wao baadhi ya wanawake.

"Kuna wanaume kadhaa wanaongea vibaya kuhusu wanawake wanaofanya upasuaji wanalenga kuwavutia wanaume, wapenzi najua mnapenda kufikiria kuwa uwepo wa mwanamke ni kukufuata kuishi kwako lakini wanawake wanafanya mambo ili waonekane mzuri, sio juu yako, "aameandika.

Kuna watu wengi maarufu duniani ambao wamefanya upasuaji wa plastiki ni pamoja na Tonto Dikeh na Runinga Khloe.

## Sky kuachia Albam yake mwezi huu

ANTHONY Sky ni msanii wa kimataifa wa afro pop, kutoka nchini Nigeria, anatarajia kuachia albam yake ya kwanza katikati ya mwezi huu.

Msanii huyo ambaye makazi yake kwa sasa yako Sweden, ameitaja Albam hiyo kuwa inaitwa 'Louda', akiwashirikisha baadhi ya wanamuziki kutoka Tanzania.

Anthony amesainiwa na lebo ya Real Definition Music ya Uingereza, amehakikisha vibao vinavyopatikana katika Albam hiyo ni moto wa kuotea mbali.



MAKALA

## KUELEKEA SIKU YA WANAWAKE

# Mpango haki LSF ulivyompokonya binti kutoka himaya ndoa ya lazima

**Na Frank Monyo**



Msichana aliyeathirika na ndoa za utotoni, akiwa katika maisha mapya. **PICHA: FRANK MONYO.**

NILIPORUDI nyumbani kutoka kwenye harusi, mama yangu alinifuata na kunijulisha kuna mtu alikuja nyumbani kuleta posa. Mama yangu hakupenda jambo hili, alimwambia baba kuwa mimi bado mdogo sana kuolewa, lakini baba hakutaka kusikia hilo. "

Hiyo ni kauli ya binti wa umri miaka 16 (jina tunalo) anayeishi Kahama Vijijini mkoani Shinyanga, anasimulia alivyonusurika kuepuka ndoa ya utotoni wakati akiwa na umri miaka 14.

Hiyo ni baada ya kupata huduma ya msaada wa kisheria kutoka kwa msaidizi wa kisheria anayefanya shughuli zake kupitia mradi wa upatikanaji haki nchini, unaofadhiliwa na Shirika la Legal Services Facility (LSF).

Anasema, masahibu hayo yalimkuta akiwa na umri wa miaka 14. Yalianza kwa kuambiwa na vijana wawili wa kiume waliofika nyumbani kwao kwa lengo la kumchumbia.

"Niliambiwa walikuja vijana wawili nyumbani wakati mimi nikiwa kwenye harusi huko Maswa na mama yangu, mmoja alikuwa amemsindikiza mwenzie na dhumuni lao halikuwa jingine, isipokuwa kuja kunichumbia," anasimulia.

Binto huyo wa anaeleza kuwa baba yake ndiye aliyepokea mahari kutoka kwa kijana huhuku akitamka: "Nakumbuka nilisafiri na mama kwenda Maswa. Huku nyuma baba yangu akapokea ng'ombe watano kama mahari yangu na akawahamisha pale nyumbani.

"Niliporudi, aliniamuru niende kwa huyo mwanamume, nilipokataa alitumia nguvu na kunifukuza nyumbani, ikabidi niende. Niliweka wazi msimamo wangu kwamba sitaki kuolewa kwa kuwa umri wangu bado mdogo,lakini baba yangu hakutaka kunielewa."

**MAISHA YA NDOA**

Anasema kuwa aliishi na mwanaume huyo kwa miezi minne, maisha yalikuwa ya mateso makubwa kwani alikuwa akilazimishwa kufanya tendo la ndoa huku akiambulia vipigo alipokataa.

Mama huyo anasema kuwa kipigo ndani ya nyumba, ilikuwa sehemu ya maisha yake, huku akiishi kwa hofu kuhusiana na uhai wake.

Hapo ilimfanya aamue tena kurudi nyumbani, lakini mwanamume huyo alizuia nguo na vitu vyake vingine kama njia ya kuendelea kumdhibiti mama huyo kubaki katika makazi hayo.

**USAIDIZI KISHERIA**

Lulu Abdallah, ambaye ni Msaidizi wa Kisheria aliyepewa elimu na Shirika la Legal Services Facility (LSF), anasimulia alivyoletewa taarifa ya binti huyo, akisimulia: "Majirani walimuona akiteseka, waliwasiliana na mimi na kunieleza kilichokuwa kinaendelea.

"Hivyo kabla ya kumhusisha mama yake, nilichukua jukumu la kulishughulikia tatizo hilo na kujaribu kumuokoa toka kwenye janga hilo. Mwanamume aliyemuoa alikuwa na umri wa miaka 25 na alimtendea unyama mkubwa.

"Ilisemekana pia kwamba alikuwa akivuta bangi na kila alipovuta, alizigeuzia nguvu zake. Kwa kusaidiana na wenzangu, tulimuita ili tulifanyie kazi suala hili na hatimaye ndoa ile ivunjwe, lakini aligoma kuja.

"Tulifanikiwa kuwapata wazazi wa pande zote mbili ingawa baba yake (binti huyo), hakutoa ushirikiano. Tulijitahidi sana na hatimaye tulifanikiwa kuwatenganisha na msichana huyu alirudi nyumbani," anaeleza Abdallah.

Anasema afya ya binti huyo ilichunguzwa na hakukutwa na tatizo lolote ikiwamo ujauzito. Hata hivyo, familia ya mwanamume ikaanza kudai warudishiwe mahari yao, lakini hawakufanikiwa, kwa sababu ndoa ile haikuwa halali na hivyo kisheria hakukuwapo haki ya kudai mahari.

**MAMA BINTI**

Mama wa binti huyo (jina tunalo), naye ana ufafanuzi wake kupitia matamshi: "Mume wangu aliondoka na wale ng'ombe, akaenda kuishi Mpanda na wake zake wengine na akaniacha niilee familia peke yangu.

"Chakula, ada za shule, mavazi na kila kitu vikabaki kuwa juu yangu. Ninafanya shughuli za kilimo kwenye eneo ambalo dada yangu alinigawia, na hivyo ndivyo tunavyomudu kuishi."

**MAFUNZO MAPYA**

Msaidizi wa Kisheria kutoka Kahama, Abdallah Abdallah anasema kuwa mwaka jana kuna tangazo lilisambazwa kwenye kata nzima, likitoa maelezo kuhusu mafunzo maalumu kwa wasichana wenye umri wa miaka 14 hadi 18, ambayo yangewapatia ujuzi kwa ajili ya kuendeleza uchumi.

Abadallah anasema, mafunzo hayo yalipoanza, msaidizi huyo alifanya utaratibu wa kumuandikisha binti huyo aweze kujijengea maisha yake ya baadaye.

"Alipokelewa na akaenda kujifunza kushonea cherehani, mradi ambao uliotoa mafunzo hayo, baadaye baada ya kumalizika kwa mradi, kila msichana alipatiwa cherehani moja, ambayo ndiyo hutumia... kumpatia kipato, " anasema.

Hivi sasa Abdallah anatumia uzoefu huo, kuwakumbusha wazazi kutoa kipaumbele kwa ustawi wa watoto wao, hasa wa kike na waache tamaa zinazokwishahatarisha maisha ya wasichana.

Pia, anakumbusha kwamba wasichana wanahitaji kujifunza, kuwa na msimamo imara na kutokubali kukatisha ndoto zao.

**MAISHA MAPYA**

"Sikutaka kuolewa, na sasa ninafurahia kazi yangu ya ufundi cherehani. Natumia ujuzi wangu kushona sare za shule na nguo zingine, ambazo ninauza na hela ninayopata inatusaidia kwenye mahitaji yetu hapa nyumbani kama vile chakula na zaidi pia kununua dawa pale mmoja wetu anapougua.

"Hitaji langu kubwa ni vitambaa ambavyo endapo nitavipata kwa urahisi vitanisaidia kushona nguo nyingi zaidi," anaeleza.

Kimsingi, ni aina ya desturi na mfumo wa maisha kandamizi, zinazozuia uwezekano wa wasichana kutimiza ndoto zao maishani na kimsingi huzuia haki zao kamili.

Pia, ni namna inayozia njia zao kuelekea kwenye haki ambazo ndiko kwenye msingi wa programu ya LSF ya upatikanaji wa haki inayoendelea nchini kote.

Ni namna gani mfumo wa maisha, mali na sheria inagusa maisha ya mwanamke, soma makala uk 16.

## KUELEKEA SIKU YA WANAWAKE

# Mila, desturi mbaya ni kaburi ukombozi wa mwanamke

**Na Mwandishi wetu**

KATIKA kuelekea maadhimisho ya Siku ya Mwanamke Duniani, mapambano ya kuhakikisha kunakuwa na usawa kati ya mwanamke na mwanaume, mila na desturi potofu ya umiliki wa mali bado yanaendelea.

Mila na desturi kwa baadhi ya makabila nchini zimetajwa kama moja wapo ya kikwazo vinavyomkandamiza mwanamke kupata haki yake katika jamii.

Wasaidizi wa kisheria wamekuwa wakishughulika na matatizo ya wanawake hasa wajane ambao wananyimwa haki zao baada ya kufariki kwa waume zao.

Mara nyingi migogoro ya aina hiyo, uibuliwa na ndugu wa mwanaume wakiamini kutokana na mila na desturi, mwanamke hana haki ya kupata urithi wala kumiliki mali.

Kwa mujibu wa Ripoti ya Shirika la Legal Services Facility (LSF) ya mwaka 2019, inaonyesha jumla ya kesi 3,848 za mirathi zilizoripotiwa kwa wasaidizi wa kisheria na kati yake 2,318, zililetwa na wanawake, ambapo 1,280 sawa na asilimia 55 zilipatiwa usuluhisho na asilimia 34 walipata mali zao.

Anna Munisi, Mkazi wa Kijiji cha Mungushi wilayani Hai, Mkoa wa Kilimanjaro ni mmoja wa wanawake waliokumbwa na makasa huo baada ya kifo cha mume wake mwaka 2008.

Anasema baada ya mume wake kufariki, ndugu wa mume walianza mikakati ya kujimilikisha mali za marehemu alizochuma nae ambapo kihalali zilitakiwa kurithiwa nae.

"Ndugu wa marehemu mume wangu walidhamiria kujinyakulia mali nilizochuma na marehemu mume wangu, niliripoti suala hili kwa mtendaji wa kijiji baada ya kunisikiliza alinielekeza kwenda ofisi za wilaya, ambapo niliunganishwa na ofisi ya wasaidizi wa kisheria," anasema Munisi.

**MTENDAJI WA KIJIJI**

Mtendaji wa Kijiji cha Mungushi, Asha Mpay, anakiri kupokea kesi hiyo na kusema suala hilo sio geni katika kijiji hicho kwani kwa utamaduni wao imezoeleka mwanamke hana haki ya kirithi mali.

"Suala la Anna halikuwa geni hapa tulipo, kwa sababu kitamaduni wanawake wanabaki wametengwa inapokuja masuala ya kurithi mali baada ya kufiwa na waume zao," anasema.

Anaongeza kuwa aliona upo umuhimu wa kumsaidia mjane huyo hasa kutokana na kwamba, aliachwa na watoto wadogo waliohitaji kwenda shule pamoja na mahitaji mengine, na hivyo msingi bora wa maisha yao ya baadaye lilikuwa jambo la muhimu.

"Nilifanya kazi mara kwa mara na shirika la wasaidizi wa kisheria kutatua mambo mbalimbali, na suala lake lilipokuja sikusita kuwasiliana na Eutropia Assenga, ambaye ni msaidizi wa masuala ya kisheria, kwa sababu nilijua kulikuwa na masuala ya kisheria yaliyohitaji kufanyiwa kazi ili apate haki zake," anasema.

**MSAIDIZI WA KISHERIA**

Assenga, anasema baada ya kukutana na majane huyo, alimwongoza taratibu zote za kisheria pamoja na kumjengea uwezo wa kukabiliana na changamoto hiyo.

"Nilifanya hivyo kwa kuwa anaelewa changamoto wanazokutana nazo wajane pale wanapohitaji kukabiliana na ndugu wa mume wenye usumbufu katika masuala ya mirathi, alinitajia mali alizochuma na marehemu ambazo ni nyumba na shamba, ambavyo kimsingi ndivyo alivyovitegemea kuweza kuishi vizuri na watoto wake,"

"Nilimsaidia Anna (mjane) kumpatia kila aina ya mwongozo, kwa sababu kulikuwa na maeneo muhimu ya mirathi, ambayo hakuyafahamu. Nilimuomba cheti cha kifo cha mume wake, muhtasari wa vikao vya ukoo, pamoja na majina ya ndugu wa karibu waliokuwa wakimsaidia katika suala hilo,"

Anasema kuwa baada ya kupata nyaraka hizo ambazo ni muhimu katika utetezi wa madai hayo, alimjulisha kuwa utaratibu mirathi husikilizwa mahakama ya mwanzo, hivyo alimsimamia kufungua shauri.

Anaongeza kuwa kwa mujibu wa sheria inavyotaka tangazo lake liliwekwa na baada ya muda uliopangwa kupita bila ya kuwepo pingamizi yoyote hatimaye alikabidhiwa mali zake mbele ya mashahidi.

**MJANE**

"Nilifanikiwakurudishiwa mashamba mawili, hekari moja hapa kijijini (Mungushi) na nyingine Kambi ya Nyuki, ambapo siyo mbali na hapa. Nilipata pia nyumba, ambayo imezungukwa na migomba kule mlimani. Unajua kabla baba mkwe wangu hajafariki, pia aliandika kwenye mirathi aliyoiacha kwamba mali hizi ni urithi wangu, lakini ndugu wengine wa mume wangu hawakuwa tayari kuheshimu hilo," anasema.

Anasema kuwa anawashukuru wasaidizi wa kisheria wanaofanya shughuli zao kupitia mradi wa upatikanaji haki nchini, unaofadhiliwa na Shirika la Legal Services Facility (LSF) kwa msaada wao kwani kwa miaka mingi alikuwa akiishi kwa wasiwasi kwa kupambania haki yake na watoto.

"Mimi ni miongoni mwa wanawake wengi ambao wangeweza kupoteza mali walizoachiwa na waume zao, lakini kwa vile msaada wa kisheria haukuwa mbali, nilipata nafasi nyingine, ambayo ilinipa manufaa makubwa binafsi na ya watoto wangu."

"Pale shambani pamoja na ndizi ninalima mahindi na maharage na hapa nyumbani nina duka dogo. Pia ninafuga nguruwe kadhaa na kuku, mifugo ambayo kwa pamoja inanisaidia katika mahitaji yangu muhimu hapa nyumbani.

"Mtoto wangu mmoja yuko chuo kikuu, mwingine kidato cha tatu na wa mwisho yuko darasa la saba, na kupitia mazao ninayolima na kuuza ninawalipia ada. Matumaini yangu ya baadaye ni makubwa kwa kuwa nimepata kilichokuwa changu na nina uhuru wa kutumia hizi mali kwa ajili ya familia yangu," anaongeza.

Anaeleza kuwa kutokana na mafanikio hayo aliweza kushiriki kwenye vipindi vya redio pamoja na kufundisha na kuelimisha jamii kuhusu kuwatumia wasaidizi wa kisheria kudai haki zao.

Anatoa wito kwa jamii kuacha utamaduni wa kale hasa ule unaowanufaisha wanaume kwa kuwakandamizawanawake.

"Ni muhimu watu waelewe kuwa, kila mmoja ana haki sawa na haki hizi lazima ziheshimiwe," anasema.



Mjane Anna Munisi akihudumia mifugo yake, ikiwa ni moja ya shughuli anazojishughulisha nazo kujipatia kipato kuhudumia watoto wake baada ya msaada wa kisheria alioupata kumwezesha kurithi rasmi mali kupitia wosia aliouacha marehemu mume wake. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Baraza la Usalama UN lashindwa kukubaliana na mzozo Tigray

**Addis Ababa, ETHIOPIA**

BARAZA la Usalama la Umoja wa Mataifa, limeshindwa kufikia tamko la pamoja kuhusu mzozo wa Tigray Kaskazini mwa Ethiopia, baada ya Urusi, China na India kuchukulia mgogoro huo kuwa suala la ndani.

Wanadiplomasia walionukuliwa na Shirika la Habari la AFP walisema nchi tatu za Afrika katika baraza hilo, Kenya, Niger na Tunisia, zimeunga mkono rasimu ya taarifa iliyoandikwa.

Kamishna wa kutetea haki katika Umoja wa Mataifa (UN), awali kulikuwa na ripoti za kusikitisha zinazoashiria huenda uhalifu wa kivita ulitekelezwa katika Jimbo la Tigray.

Michelle Bachelet aliangazia visa vya unyanyasaji wa kijinsia, mauaji ya kiholela na uharibifu mkubwa ulifanywa katika eneo hilo.

Ofisi ya Umoja wa Mataifa ya kutetea haki inataka kupewa idhini ya kuchunguza ripoti za ukatili uliotekelezwa na majeshi ya Ethiopia na Eritrea, wapiganaji wa Tigray People's Liberation Front na vikosi vya jimbo la Amhara. **BBC**




Papa Francis, akipunga mkono kabla ya kuanza safari kuelekea nchini Iraq, katika Uwanja wa Ndege wa Leonardo da Vinci-Fiumicino, mjini Roma, Italia, jana. **PICHA/REUTERS**

# Papa Francis atembelea Iraq

**Roma, ITALIA**

PAPA Francis ameanza ziara ya siku nne ambayo ni ya kihistoria Iraq licha ya hatari za usalama na virusi vya corona.

Papa Francis alisafiri jana katika ziara ya kwanza rasmi nchini humo na safari yake ya kwanza ya kimataifa tangu kuzuka kwa corona.

Safari hiyo inakusudiwa kuihakikishia jamii ya Kikristo inayopungua ya Iraq na kukuza mazungumzo ya kidini.

Papa atakutana na Kiongozi wa Waislamu wa dhehebu la Kishia anayeheshimiwa sana, na kufanya sala huko Mosul na kuhudhuria misa katika uwanja wa michezo.

Alisisitiza kufanya ziara hiyo licha ya ongezeko jipya la maambukizi ya Covid-19 nchini Iraq na hofu dhidi ya usalama wake.

Saa kadhaa baada ya shambulio la roketi dhidi ya kambi inayokaliwa na wanajeshi wa Marekani siku ya Ijumaa, Papa alisema Wakristo wa Iraq hawawezi kuvunjwa moyo kwa mara ya pili. Mkuu huyo wa Kanisa Katoliki la Roma analenga kuwatia mayo Wakristo wanaoteswa na kushinikiza amani katika mikutano na viongozi wa kisiasa na kidini.

Kutokana na sababu za kiusalama na kuongezeka kwa viwango vya maambukizi ya Covid-19, Papa mwenye umri wa miaka 84, atadhibiti mwonekano wake hadharani, mwandishi wetu anasema.

Pia kuna hofu ziara hiyo ikawa chanzo cha kuenezwa kwa virusi.

Akiwahutubia watu wa Iraq kupitia ujumbe wa video mkesha wa safari yake, Papa Francis alisema "nakuja kama hujaji, msafiri anayetubu, kumwomba bwana msamaha na upatanisho baada ya miaka kadhaa ya vita na ugaidi, kuomba faraja kutoka kwa Mungu na uponyaji wa mioyo wa majeraha".

"Nakuja miongoni mwenu pia kama hujaji wa amani...kutafuta ushirika unaotokana na hamu ya kuomba pamoja na kutembea pamoja, pia na ndugu na dada zetu wa dini nyingine katika nyayo za Baba Abrahamu, ambaye anajiunga na familia moja ya Waislamu, Wayahudi na Wakristo."

Papa John Paul wa Pili, alifuta mpango wa safari yake nchini humo mwisho wa mwaka 1999 baada ya mazungumzo kati yake na rais wa wakati Iraq wakati huo Saddam Hussein kuvunjika.

Ndani ya miongo miwili tangu wakati huo, moja ya jamii ya zamani ya Wakristo duniani imeshuhudia idadi yake ikipungua kutoka milioni 1.4 hadi karibu 250,000.

**TRT**

# Sokwe wapewa chanjo corona

**San Diego, MAREKANI**

SOKWE kadhaa katika hifadhi ya wanyama ya San Diego, wamepewa chanjo ya majaribio ya Covid-19 zilizotengenezwa kwa ajili ya wanyama baada ya mlipuko wa ugonjwa huo kutokea miongoni mwa sokwe hao.

Sokwe wanane katika hifadhi hiyo walikuwa wa kwanza duniani kupatikana na virusi vya corona mwezi Januari.

Kwa sasa wanaendelea kupokea matibabu.

Wahifadhi wa wanyama wana wasiwasi kuhusu tisho la ugonjwa wa corona kwa sokwe wa jadi.

Wana wasiwasi hasa juu ya baadhi ya spishi za sokwe wanaokabiliwa na tishio la kuangamia.

Wanyama wengine waliopatikana na virusi vya corona ni pamoja na simba katika mbuga ya Barcelona huko Barcelona na duma katika hifadhi ya wanyama ya Bronx huko New York.

**BBC**

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## TANGAZO TANGAZO
## MNADA WA NYUMBA

**Fagio Brokers** kwa amri tuliyopewa na Mahakama ya Mwanzo iyunga tutauza kwa mnada wa hadhara nyumba moja iliyopo mtaa wa Inyala kata ya Iyunga mali ya waliokuwa wanandoa **ALPHA MPONZA AGUSTINO NA JESCA JAMES TEBUYE,** Mnada utafanyika siku ya jumatatu tarehe **08/03/2021 kuanzia saa 4;00 asubuhi.**

**MASHARTI YA MNADA**

1. Mshindi atalipa 25% ya bei na baki ilipwe ndani ya siku 14 tangu tarehe ya mnada Kushindwa kulipa baki hiyo fedha hazitarudishwa na mnada utarudiwa
2. Mnunuzi atapewa hati ya manunuzi (Certificate of sale) na mahakama kama mmiliki halali wa nyumba hiyo

**KWA MAWASILIANO PIGA SIMU**
**0754 368 000**

## VACANCY ANNOUNCEMENT.

EXPERIENCED

**AGRICULTURAL SUPERVISOR**

NEEDED AT AN NGO BASED IN KIBAHA PWANI REGION.

**SEND YOUR CV THROUGH THIS NUMBER 0683786313.**

*NOTE; APPLICANT MUST BE IN POSSESION OF DIPLOMA OR DEGREE IN AGRICULTURE*

## KUPOTELEWA NA KADI YA GARI

**SEARCH FOR COMMON GROUND** ANATANGAZA KUPOTELEWA NA KADI YA GARI YENYE NAMBA ZA USAJILI **T 258 APR** AINA YA **LANDROVER TID**. KWA YEYOTE ATAKAYEIONA ATOE TAARIFA KITUO CHOCHOTE CHA POLISI.

TAARIFA YA POLISI:

**KAH/TR/RB/104//2021.**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**ELIESH WILBARD LEMA** ANATANGAZA KUPOTELEWA NA KADI YA GARI YENYE NAMBA ZA USAJILI **T 807 BJR** TOYOTA **COASTER.** YEYOTE ATAKAYEIONA ATOE TAARIFA KITUO CHOCHOTE CHA POLISI.

TAARIFA YA POLISI:

**DAR/URA/RB/108935/2021.**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**KATIKA MÀHAKAMA YA MWANZO MJINI ILIYOPO MOROGORO**

**TANGAZO LA KUITWA SHAURINI**

**SHAURI LA MADAI NO. 73/2021**

**MDAI DENIS ME THEW MSANZYA**

**DHIDI YA**

**MDAIWA ANOSISYE MWASYEBA**

**Kwa:**
**ANOSISYE MWASYEBA**
**K.K. OCS POLISI POLISI(W)**
**MOROGORO**

**Ombi la Mdai DENIS METHEW MSANZYA**
**Madai ya Pesa 1,205,000/=(MILIONI MOJA LAKI MBILI NA ELFU TANO TU)**

Unatakiwa kuhudhuria hapa Mahakamani katika shauri tajwa hapo juu bila kukosa. Shauri limepangwa kusikilizwa mnamo tarehe 17 mwezi 03 mwaka 2021 saa 2:30 Asubuhi.
Angalia kama hukuhudhuria/hamkuhudhuria siku iliyotajwa hapo juu. Màhakama ikithibitisha kama umepokea/mmepokea kuitwa shaurini, hii itaweza kutoa hukumu kuwa umeshindwa/mmeshindwa.
Hati hii yatolewa kwa amri yangu na chapa ya mahakama hii leo tarehe 04 mwezi 03 mwaka 2021

**ROYAL RUNNER'S & GENERAL SUPPLIIES (T) LTD DODOMA**

**MAHAKAMA KUU YA TANZANIA**

**(COMMERCIAL DIVISION)**

**MAHAKAMA YA BIASHARA DAR ES SALAAM**

**TANGAZO LA KUUZA YARD KWA NJIA YA MNADA WA HADHARA ILIYOPO KIZOTA**

**MISC.COMMERCIAL CAUSE NO. 53 OF 2020.**

**ZHENGHZZHOU GIANT ELECTRIC EQUPMENT CO. LTD.... DECREEE HOLDER**

**VERSUS**

**NIPO GROUP LTD (KELLOGG CONSTRUCTION & NIPO AFRICA ENGG.CO.JV) .... JUDGEMENT DEBTOR.**

Kwa idhini tuliyopewa na mahakama ya biashara Dar es salaam kesi NO.53/2020 Tutauza YARD ya mdaiwa **NIPO GROUP LTD (KELLOGG CONSTRUCTION & NIPO AFRICA ENGG.CO.JV) .... JUDGEMENT DEBTOR iliyopo Kizota DODOMA** Mjini ili kufidia deni analodaiwa na **ZHENGHZZHOU GIANT ELECTRIC EQUPMENT CO. LTD.... DECREEE HOLDER**. Mnada huo utafanyika tar 06/04/2021 saa nne asubuhi maeneo ya Kizota.

**Kwa mawasiliano 0713913150 au 0688729841.**

**OFISI ZA MATANGAZO**

**MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,**

**PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 745 700 710.**

**E-mail: advertise@guardian.co.tz, website: www.ippmedia.com**

**Kwa Habari Motomoto**

usikose Gazeti lako

la Nipashe kila siku

Tupigie

0782253676

Nipashe
www.ippmedia.com MWANGA WA JAMII

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

# HADITHI

# Lazima Apatikane-11

MAUAJI ya kutisha yanatokea ndani ya gesti moja maeneo ya Kigogo jijini Dar es Salaam. mfanyabiashara Burhan anauawa ndani ya gesti ya Tukutane, akiwa na msichana mmoja mrembo aitwaye Mwanaidi. Polisi wanawakamata watu wote waliokutwa humo, pamoja na wafanyakazi wa gesti hiyo kwa ajili ya mahojiano. Lakini inaonekana muda ambao walikuwapo wapenzi hao hakukuwa na mteja mwingine yoyote zaidi yao. Baada ya mahojiano ya kina, inaonekana kabisa kuwa Mwanaidi ndiyo muuaji. Je, ni kweli? Kwa nini alimuua mpenzi wake wakiwa wamejifungia chumbani?

Fuatilia hadithi hii kwa makini ambayo mbali na kukutia simanzi, furaha na kukuburudisha, pia itakufundisha, elimu na kufunulia mambo ambayo hukupata kuyafikiria kabla.

**Na Adam Fungamwango, (0716 350534)**




"Kwa kukusaidia tu Mwanaidi ni kwamba kifo kile alikitaka mwenyewe mpenzi wako. Nisingemuua kama angemaliza kazi na kuzileta pesa ubaoni kila mtu akachukua mgao wake. Baada ya kuwapa kazi ya kwenda kupora pesa kwa mchongo na mchoro nilioletewa na Tika, huyu mfanyakazi wa benki ambaye umemuua leo kwa sumu, nilimwambia azilete saiti. Yeye akataka kunizidi akili. Walipozipora na wenzake watatu, badala ya kuzileta, yeye akawaua wenzake kwa lengo la kutoroka na pesa zote. Maiti akazitupa Kimara. Nadhani ndiyo akaja kwako. Lengo ikiwa akitoka pale gesti akimbie na pesa zote. Hakujua kuwa mimi kazi hizi za ujambazi nilizianza tangu nina miaka 18. Wakati wanapora mpaka anafanya mambo yake, mimi nilikuwa nawafuatilia bila kujua na gari yangu. Na mwisho wa siku nikamwona ameingia na mwanamke kwenye gesti ya Tukutane Kigogo, ambaye ni wewe. Ndiyo nikafanya vile bila kuacha alama yoyote wala ushahidi na kila kiumbe duniani kikajua kuwa wewe ndiye muuaji." Akasita na kuachia tabasamu kana kwamba alikuwa amefanya jambo la kishujaa.

"Labda unajiuliza, niliiingiaje mle ndani na nilimuuaje? Nitakueleza kila kitu, kwa sababu leo hii mmoja atakuwa marehemu na mwingine atabaki duniani akiishi kwa raha. Ni mchezo mdogo sana."

Alisema huku akimwangalia Mwanaidi kwa namna ya kama kujionyesha kwamba yeye ni mtaalamu na shujaa.

"Baada ya kuondoka kule Kimara alipotupa maiti za wenzake, alikufuata wewe nyumbani hapa. Na ndiyo mwanzo wa mimi kupafahamu hapa. Hakukukuta. Akaenda hadi saluni kwako, akakukuta. Mkachukuana na kuongozana hadi kwenye gesti ya Tukutane," alisema na kumeza mafunda kadhaa ya mate.

Wakati huo Mwanaidi macho yalikuwa yamemtoka. Alikuwa akiisikiliza hadithi mbaya kwenye historia yake, iliyomuua mpenzi wake Burhan. Mauaji ambayo yeye anatuhumiwa nayo, kiasi kwamba ana kesi ya mauaji na sasa yupo nje tu kwa dhamana.

"Kwenye gesti kuna sehemu tatu za kuingilia. Kwanza kwenye gesti kuu, ambapo wateja wanaweza kuingia kwa kutumia magari. Pili mlango wa kawaida ambapo wapenzi wasio na usafiri ndiyo huingilia. Halafu kuna mlango wa tatu. Huu uko kama mlango wa dharura hivi. Uko nyuma ya gesti hiyo. Huu ni mdogo na mwembamba, lakini pia umewekwa kwenye njia ya vichochoroni. Ni maalum kwa watu ambao wanakwenda pale, lakini ni wake za watu au waume za watu. Nyinyi mliingia kwenye mlango wa kawaida, mimi niliingia kwenye mlango wa dharura," alisema.

Pamoja na kwamba ilikuwa ni hadithi mbaya, lakini Mwanaidi alitaka kujua ni jinsi gani au ufundi gani alitumia Martin kuingia pale kama mzimu na kuua, asionekane na mtu yoyote yule, kiasi kwamba hata askari polisi wameshindwa hata kuhisi tu kama huenda kulikuwa na mtu mwingine aliyefanya hivyo, badala yake kesi kumwelemea yeye.

"Nilichungulia kwanza, nikamuona mhudumu wa kaunta akila chakula. Baadaye akatoka pale alipokuwapo kaunta. Muda huo huo kama umeme nikapita na kwenda kwenye ukumbi ambao una vyumba ambavyo nyinyi mliingia. Nilisikia sauti kwenye chumba namba 17, nikajua mmeingia humo, nikapitiliza hadi mwisho wa ukumbi ambapo kulikuwa na chumba ambacho walisahau kufunga, nikaingia. Nilikuwa nasubiri mfunge mlango ili mimi nije kufungua kwa ufunguo malaya ambao unafungua kila kufuli au kitasa." Martin aliendelea kuweka wazi jinsi alivyofanya mauaji ya Burhan.

"Tena una bahati. Usingekufa leo. Ningekuua siku ile ile na mpenzi wako. Lengo ni kuueni wote wawili. Na msingejua nini kimewaua kwa sababu nilikuwa nasubiri muanze kilichowapeleka. Una bahati baadaye ukatoka. Lakini niliwasikia mkitumana soda, nikajua kabisa unakwenda kununua vinywaji, kimoyomoyo nikasema hata hivyo ni poa tu kwa sababu niliyemtaka ni Burhan na si wewe."

Martin aliongea na kuangalia saa yake ya mkononi, akiwa bado amekamatia bastola yake.

"Mkakati na akili ikabadilika, nikaona sasa Burhan nimuue kwa kisu ili wewe ndiyo ujulikane kama muuaji, kwa sababu nilijua utarudi baadaye na soda zako na kukuta maiti. Ningemuua kwa bastola, kipigo au kabali, askari polisi wengetia shaka kama wewe ndiye muuaji, kwani mwanaume jasiri kama yule hawezi kuuawa kwa kupigwa au kabali na mwanamke, lakini kisu ni rahisi kwa sababu wangehisi umemuua alipolala usingizi kama wanavyoamini sasa. Bastola ingekuwa ngumu kwa sababu hujawahi kumiliki, hivyo wangemtafuta mtu mwingine, lakini hii ya kukung'ang'ania wewe nilifanya kwa makusudi. Aina ya uuaji niliibuni ili kuwapoteza lengo polisi wakukamate wewe."

"Nilichofanya ulipoondoka tu ni kuingia ndani kiurahisi kwa sababu mlango haukufungwa. Alikuwa hajajiandaa kumuona mtu kama mimi. Alishtuka, lakini kabla hajafanya lolote nilimpiga ngumi ya uso akaangulia kitandani, nikammalizia kwa kumshindilia na kisu mara nne kifuani, nilitoka bila kuonekana na yoyote yule mle ndani." Alinyamaza na kuonekana kama amemaliza au anasubiri yamwingine.

"Saa zimekwenda sasa, natakiwa nitoke hapa, kwa heri Mwanaidi." Alisema huku akiwa anakoki bastola yake, tayari kwa kuitumia. Ni wakati ambao Mwanaidi alikuwa amefumba macho akisubiri zawadi yake risasi ya kichwa kutoka kwa Martin.

Alisikia sauti kali. Sauti iliyotaka hata kuziba masikio yake. Ni sauti kama kuna kitu chuma au jiwe kubwa limepiga juu bati na kutoa mlio wa kutisha.

Alihisi kuwa huenda hiyo ndiyo sauti inayoashiria mtu anavyokata roho na kufa, akielekea kuzimu.

Alitaka kusema "Mama nakufa..." Lakini sauti haikutoka.

**Itaendelea Jumamosi**

## HABARI MICHEZO



# SOLSKJAER
## AMEFANYA KAZI NZURI UNITED -WOODWARD

**MANCHESTER, England**

MAKAMU Mwenyekiti Mtendaji wa Manchester United, Ed Woodward, amepaza sauti ya "maendeleo" ya kikosi hicho chini ya Kocha, Ole Gunnar Solskjaer msimu huu.

Woodward amesema United imekuwa na maendeleo mazuri dimbani na kibiashara kwa kipindi cha mizei 12 iliyopita licha ya uwapo wa mlipuko wa virusi vya corona.

Woodward amebainisha kazi kubwa iliyofanywa na Solskjaer kwa kikosi hicho, ambacho kipo nafasi ya pili kwenye msimamo wa Ligi Kuu England, kikipitwa pointi 14 na vinara Manchester City.

United walicheza mchezo wao wa sita wa sare msimu huu - baada ya Jumatano kutoka suluhu na Crystal Palace.

Miamba hao wa Ligi Kuu England pia wametoka sare tatu za mfululizo za suluhu kwenye mashindano yote kwa mara ya kwanza tangu Oktoba, mwaka 2015 wakiwa chini ya Louis van Gaal.

"Maendeleo yaliyofanwa na Ole na wachezaji msimu huu yako wazi kabisa, kwani tumekuwa bora dimbani na nje ya uwanjani," alisema Woodward akiwaambia waandishi wa habari.

United - haijatwaa ubingwa wa Ligi Kuu England tangu msimu wa 2012-13 - pia wapo kwenye robo fainali ya Kombe la FA na wamefuzua hatua ya 16 kwenye Ligi ya Europa, huku pia wamefuzu nusu fainali ya Kombe la EFL.

# Inter yatangaza kuachana na Pirelli

**MILAN, Italia**

MKURUGENZI Mtendaji wa Kampuni ya kutengeneza matairi ya gari Pirelli, Marco Tronchetti Provera amethibitisha kwamba, Inter Milan itabadilisha wadhamini wao kuanzia msimu ujao.

Pirelli imekuwa mdhamini wa Inter Milan kwa miaka 27 iliyopita na huu ni msimu wa mwisho ambapo jina lake litaonekana tena kwenye vifaa vya mchezo vya Nerazzurri.

"Tunafanya mazungumzo na Antonello, Marotta na wakurugenzi wengine wa Inter Milan.

"Hatutakuwa wadhamini wa vifaa vya Inter tena, lakini uhusiano wetu na klabu utaendelea, " alisema Tronchetti akiwaambia waandishi wa habari.

Mapema wiki hii, Kampuni ya Suning ya China ilithibitisha itawatasaidia kifedha Inter, ingawa wanatafuta washirika wanaofaa na Tronchetti hana wasiwasi wowote juu ya hatima ya klabu hiyo.

"Lazima tushikamane na ukweli, tuliwasaidia na kampuni ilithibitisha kujitolea kwake kwa Inter.

"Kwa hivyo, nadhani lazima kuwe na njia nyingine ya kawaida kwa ajili ya kuiendeleza klabu hiyo," alisema.




# Tuchel aionya Chelsea



**LONDON, Engand**

THOMAS Tuchel ana "furaha kubwa" kwa ushindi wa 1-0 kwenye Ligi Kuu England dhidi ya Liverpool, lakini ameionya Chelsea kama inaweza kuwa kwenye kiwango bora katika mbio za kumaliza kwenye nne bora.

Mason Mount alifunga bao hilo pekee kwenye mchezo huo wakati Blues hao wakiwafanya Liverpool kupoteza mchezo wao wa tano mfululizo kwenye dimba lake la nyumbani la Anfield kwa mara ya kwanza katika historia.

Kiungo wa England, Mount alimalizia vizuri pasi aliyopewa kipindi cha kwanza na kuifanya Chelsea kuendeleza ushindi kwa mechi 10 tangu ujio wa Tuchel aliyechukua nafasi ya Frank Lampard aliyetimuliwa Januari, mwaka huu na wapo nafasi ya nne katika msimamo.

Chelsea wamewapita Liverpool pointi nne ambapo wapo nafasi ya saba, na hivyo wanaweza kukosa kufuzu Ligi ya Mabingwa Ulaya msimu ujao.

Tuchel alisema: "Nina furaha kubwa. Nikiwa mkweli bado ninajutia sare tuliyopata dhidi ya Southampton kwa sababu sikufurahia kupoteza pointi mbili na tukashuka.

"Lakini kwa ujumla nina furaha. Tangu siku ya kwanza niliyotua klabuni hapa niliona mambo mengi mazuri.

"Lakini sasa lililopo mbele yetu ni kuhakikisha tunamaliza kwenye nne bora, maana ushindani ni mkubwa sana kwa sasa.

"Tunatakiwa kuendelea kuwa kwenye kiwango hiki, kwenye kila mchezo uliopo mbele yetu.

Tuchel na Chelsea mchezo wao unaofuata ni dhidi ya Everton waliopo nafasi ya tano utakaopigwa Jumatatu.

## HABARI MICHEZO



# KIWANGO CHA DELE CHAMKUNA MOURINHO

**LONDON, England**

JOSE Mourinho ameweka wazi, Dele Alli alistahili kuanza katika kikosi cha Tottenham Hotspur dhidi ya Fulham baada ya kufanya kazi nzuri katika wiki za hivi karibuni - na alifurahia kile alichokifanya wakishinda 1-0, juzi Alhamisi.

Alli alitajwa kwenye kikosi cha kwanza cha Spurs kwa mara ya pili kwenye mchezo wa Ligi Kuu England msimu huu, na kiungo huyo alicheza kwa dakika 67 kabla ya nafasi yake kuchukuliwa na Moussa Sissoko.

Mchezaji huyo wa kimataifa wa England alitengeneza nafasi mbili na kuendelea kuonyesha ubora wake kwenye mchezo huo.

Mara baada ya mchezo huo, Mourinho alisema Alli alistahili kuanza na haikuwa "zawadi" kwake.

"Alistahili. Haikuwa zawadi kwake, yalikuwa ni matokeo ya kazi nzuri aliyofanya tangu amerudi tena kwenye timu.

"Nina furaha kubwa kwamba alifanya kazi nzuri kwenye timu na amekuwa fiti na tayari kucheza kila mchezo," alisema Mourinho akiwaambia waandishi wa habari.

"Alikuwa anatoa vitu muhimu kwetu. Alifanya vizuri kwenye Ligi ya Europa. Alifanya vizuri sana dimbani dhidi ya West Ham na Burnley, hivyo ana stahili."

# WIJNALDUM AKUBALI KUTUA INTER MILAN

**MILAN, Italia**

KIUNGO wa Liverpool, Georginio Wijnaldum amekubali kujiunga na timu ya Inter Milan ya Italia.

Kwa mujibu wa ripoti za vyombo vya habari vya Italia, Wijnaldum ameamua kwenda kukipiga kwa vinara hao wa Ligi Kuu Italia, Serie A, mara mkataba wake utakapomalizika mwishoni mwa msimu huu.

Mkataba wa kiungo huyo wa Kimataifa wa Uholanzi, unamalizika mwishoni mwa msimu huu na atakuwa huru kuondoka pale katika dimba la Anfield.

Wijnaldum pia alikuwa anahusishwa na kuhamia Barcelona, ambako alikuwa akitajwa kuwa atajiunga na kocha, Ronald Koeman ambaye alimnoa kwenye timu ya taifa.

Koeman ametajwa ni shabiki wa Wijnaldum na alikuwa anamtaka kwa ajili ya kuimarisha kikosi cha Barcelona.

Lakini Inter pia inamtaka Mholanzi huyo na mkurugenzi wa michezo wa klabu hiyo, Guiseppe Marotta, kufanya hatua ya kumsaini mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 30.

Kwa mujibu wa ripoti Wijnaldum mwenyewe tayari amefanya mazungumzo binafsi na Inter na wamekubaliana kuhusu maslahi yake.

Kocha wa Liverpool, Jurgen Klopp, siku zote alikuwa akisisitiza kwamba, atajaribu kumshawishi Wijnaldum kubaki, lakini sasa inaonekana jitihada zake zimegonga mwamba.

# BARCELONA KUCHAGUA RAIS KESHO

**BARCELONA, Hispania**

KLABU ya Barcelona ya Ligi Kuu Hispania, LaLiga, inatarajia kufanya uchaguzi wake wa nafasi ya Urais hapo kesho Jumapili.

Uchaguzi huo unafanyika wakati bado kukiwa hakujajulikana kuhusu majaliwa ya nahodha wao Lionel Messi ambaye mkataba wake unamalizika mwishoni mwa msimu huu.

Kabla ya kuanza kwa msimu huu, Messi aliwasilisha maombi ya kutaka kuondoka klabuni hapo, kabla ya kuamua kubaki.

Awali uchaguzi huo ulikuwa ufanyike Januari 24, mwaka huu lakini ukasogezwa mbele hadi kesho kutokana na mlipuko wa virusi vya corona.

Katika kampeni za uchaguzi huo, jina la Messi lilitawala kwa wagombea wote, kila mmoja akijigamba kwamba ana uwezo wa kumbakiza nyota huyo wa kimataifa wa Argentina.

Uchaguzi huo una wagombea watatu ambao ni Joan Laporta, Victor Font na Toni Freixa.

Laporta, ambaye hapo awali aliwahi kuwa rais wa Barcelona kutoka 2003 hadi 2010, anapewa nafasi kubwa ya kushinda, akifuatiwa na Font na Freixa.

Jordi Farre, Xavier Vilajoana, Agusti Benedito, Luis Fernandez Ala na Pere Riera walikuwa wameondolewa kwenye kinyang'anyiro hicho baada ya kushindwa kufikia kizingiti cha saini 2,257.

## HABARI MICHEZO

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA




# KLOPP: LIVERPOOL MAMBO NI MAGUMU

Yapoteza mechi ya tano nyumbani na kujiweka katika hatihati ya kumaliza kwenye nafasi...

**LIVERPOOL, England**

KOCHA wa Liverpool, Jurgen Klopp, amesisitiza kupoteza mchezo wa Ligi Kuu England dhidi ya Chelsea ni "pigo kubwa" kwa matumaini ya klabu hiyo kumaliza kwenye nne bora.

Liverpool walijikuta wakifungwa na Chelsea bao 1-0 katika mchezo wa juzi Alhamisi katika dimba la Anfield na hivyo kuwa kwenye wakati mgumu wa kutetea taji hilo msimu huu.

Wakiwa wametoka kutwaa taji la Ligi Kuu England msimu uliopita baada ya miaka 30, Liverpool sasa imepoteza mechi tano zilizopita nyumbani zikiwa nyingi zaidi katika historia ya klabu hiyo.

Liverpool sasa wapo nafasi ya saba kwenye msimamo wa ligi hiyo, wakiwa wamepitwa pointi nne katika mbio za nne bora na wakipitwa pointi 22 na vinara wa Manchester City.

"Ni pigo kubwa," alisema Klopp akiiambia Sky Sports.

"Ingawa bado mechi zipo, lakini huwezi kuzungumzia ubingwa wakati unapoteza mechi nyingi, huna nafasi ya kwenda katika mashindano ya Ligi ya Mabingwa Ulaya.

"Tunatakiwa kushinda mechi zote na tunajua kwamba tutafanya kazi ya ziada, lakini kwa usiku ule (juzi) lilikuwa pigo kubwa sana kwetu."

Liverpool itashuka tena dimbani kesho Jumapili kucheza dhidi ya Fulham wakati Manchester City yenyewe itaikaribisha Manchester United kwenye Uwanja wa Etihad.

## KWA UFUPI

**KONATE ANUKIA ARSENAL**

ARSENAL ni miongoni mwa klabu kadhaa zinazoangalia uwezekano wa kumsajili mchezaji wa safu ya ulinzi wa timu ya RB Leipzig, Ibrahima Konate mwenye umri wa miaka 21. ***(Standard).***

**BRUNO MAMBO SAFI**

KIUNGO wa kati wa Manchester United, Bruno Fernandes mwenye umri wa miaka 26, yuko tayari kusaini mkataba mpya ambao utaongeza mshahara wake mara dufu na kuweza kupata malipo ya takriban pauni 200,000 kwa wiki. ***(Sun)***

**ELMOHAMADY NJIA MOJA**

MLINZI wa Misri, Ahmed Elmohamady mwenye umri wa miaka 33, ataondoka Aston Villa kwa mkataba usio na malipo msimu huu, huku klabu hiyo ikiwa haina mipango ya kumpatia mkataba mpya. ***(Football Insider)***

**KOULIBALY ASHUSHWA DAU**

KLABU ya Napoli imepunguza kiwango cha fedha walizokuwa wanataka kama ada ya kumuuza mlinzi wake, Kalidou Koulibaly hadi kufikia euro milioni 45, huku Bayern Munich wakiaminiwa kuwa mbele ya Liverpool na Manchester United katika mbio za kuwania saini ya nyota huyo wa kimataifa wa Senegal. ***(Il Mattino - in Italian)***

**LEICESTER YASHITUKA**

LEICESTER City imefikia pazuri kuhusu mazunguzo ya kumwongezea mkataba kiungo wake, Harvey Barnes mwenye umri wa miaka 23, ambaye amekuwa anawindwa na Liverpool na Manchester United. ***(Sunday Mirror)***

**NEUHAUS ANAJIAMINI**

KIUNGO wa Borussia Monchengladbach, Florian Neuhaus, mwenye umri wa miaka 23, amesema hana wasiwasi kuhusu majaliwa yake, licha ya kuhusishwa na klabu za Ligi Kuu England, Tottenham na Liverpool. ***(football.london)***

**VARANE KIMEELEWEKA**

REAL Madrid itatoa ofa kwa mlinzi wa Ufaransa, Raphael Varane, mwenye umri wa miaka 27, kipindi cha majira ya joto ili kumwongezea mkataba wake unaomalizika mwaka 2022. ***(AS, via Mail on Sunday)***

**ODERGAARD KUNG'ARA**

REAL Madrid inaamini kiungo wa kimataifa wa Norway mwenye umri wa miaka 22, Martin Odergaard, ambaye anacheza kwa mkopo kule Arsenal, ana nafasi kubwa kwa baadaye kwenye kikosi chao. ***(Marca)***

**SIMA ATAJWA EVERTON**

EVERTON inamfuatilia fowadi wa Everton na Senegal, Abdallah Sima mwenye umri wa miaka 19, ambaye anaichezea Slavia Prague. ***(Football Insider)***

**JOSEPH SOKONI**

ARSENAL, Celtic na Rangers ni miongoni mwa klabu zinazowania kumsajili straika wa Wigan na Scotland, Kyle Joseph, mwenye umri wa miaka 19, ambaye mkataba wake unamalizika kipindi cha majira ya joto kinachokuja. ***(Sunday Mirror)***

## HABARI MICHEZO




Washindi watatu kati ya watano waliofanikiwa kushinda zawadi ya televisheni, Innocent Mchino (kushoto), Amani Ephrain (katikati) na Godbless Mboya wakiwa na moja ya zawadi waliyokabidhiwa na Mkurugenzi wa Kampuni ya Tatol, Jeanfrancois Schoepp, (hayupo pichani) baada ya kubashiri kwa usahihi timu mbili zilizoingia nusu fainali ya Tatol CHAN 2020 huko Cameroon hivi karibuni. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# YANGA HAIJASHINDA CCM MKWAKWANI TANGU 2016

**Na Adam Fungamwango**

KIPIGO cha mabao 2-1 ilichokipata Yanga katika mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara iliyochezwa juzi kinaifanya timu hiyo kufikisha mwaka wa sita bila kupata ushindi wowote kwenye Uwanja wa CCM Mkwakwani Tanga ikicheza dhidi ya wenyeji Coastal Union.

Takwimu zinaonyesha mara ya mwisho Yanga kushinda kwenye uwanja huo ilikuwa ni Februari 4, mwaka 2015, ilipoichapa Coastal Union bao 1-0, kupitia kwa beki wa kati wakati huo, Nadir Haroub 'Cannavaro' dakika ya 11 na kuwa bao pekee kwenye mechi hiyo ya msimu wa Ligi Kuu Bara 2014/15.

Kipigo hicho pia kilihitimisha timu hiyo kucheza mechi 21 bila kupoteza msimu huu na mechi 33 za Ligi Kuu Tanzania Bara kucheza mfululizo bila kupoteza tangu msimu uliopita.

Hata hivyo, kati ya msimu hiyo sita, miwili Coastal Union ilikuwa imeshuka daraja, hivyo timu hizo hazikukutana msimu wa 2016/17 na 2017/18, hadi wa 2018/19, iliporejea tena katika Ligi Kuu.

Hii ina maana kuwa Yanga imecheza na Coastal Union kwa msimu minne kwenye uwanja huo bila ushindi, ikipoteza miwili na kutoka sare misimu miwili.

Baada ya kushinda bao 1-0 msimu wa 2014/15, msimu uliofuata 2015/16, Yanga ilichapwa mabao 2-0, Januari 30, 2016, mabao ya Coastal Union yakifungwa na Miraji Adam na Juma Mahadhi ambaye baadaye alihamia kwa Wanajangwani hao.

Msimu wa 2018/19, Coastal Union iliporejea tena Ligi Kuu, ilitoka sare ya bao 1-1 dhidi ya Yanga, wageni wakipata goli kupitia kwa Deus Kaseke wakati nyota wa zamani wa Simba, Haji Ugando aliifungia Coastal katika mechi iliyochezwa Februari 3, mwaka juzi.

Mechi nyingine iliyozikutanisha timu hizo ilichezwa Februari 23, mwaka jana, katika msimu wa 2019/10 ambapo dakika 90 zilimalizika kwa matokeo ya sare ya bila kufungana.

## Serengeti Boys waahidi neema

**Na Saada Akida**

KOCHA Mkuu wa Timu ya Taifa ya Vijana ya umri chini ya miaka 17 (Serengeti Boys), Hababuu Ali, amesema kikosi chake kimepata maandalizi mazuri kwa ajili ya kushiriki fainali za Kombe la Mataifa ya Afrika (AFCON U-17), zinazotarajiwa kufanyika kuanzia Machi 14, mwaka huu nchini Morocco.

Akizungumza na gazeti hili jijini juzi kabla ya kikosi hicho kusafiri kuelekea Morocco, Hababuu alisema wameamua kwenda mapema nchini humo ili kupata nafasi ya kuzoea mazingira na kucheza mechi mbili za kirafiki ikiwamo dhidi ya wenyeji.

Hababuu alisema mwaka huu wamejipanga imara kuhakikisha wanafanya vizuri na hawataki kuona wanarudia makosa yaliyojitokeza kwenye fainali za mwaka 2019 ambapo walipoteza mechi zote.

Alisema malengo ya Serengeti Boys mwaka huu ni kusonga mbele na vilevile kukata tiketi ya kushiriki fainali zijazo za Kombe la Dunia.

"Tumefanya maandalizi ya kutosha na kitendo cha kuwahi kwenda Morocco kwa ajili ya kupata mechi za kirafiki ikiwamo dhidi ya wenyeji itaendelea kunipa mwanga wa kufanyia kazi mapungufu yaliyopo katika kikosi chetu," alisema Hababuu.

Alisema hakuna kundi rahisi katika mashindano hayo huku akisema nafasi ambayo Tanzania na Uganda wamepata kutoka Afrika Mashariki ni ya kujivunia na wanatarajia watuwakilisha vizuri.

Tanzania imepangwa Kundi B, pamoja na timu za Algeria, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC), na Nigeria.

# Shabiki wa Simba ashinda M-Bet

**Na Mwandishi Wetu**

SHABIKI wa Simba na Liverpool, Joel Mtalamu ameshinda zawadi ya Sh. milioni 78.2 baada ya kubashiriki kwa usahihi matokeo ya michezo 12 ya mpira wa miguu ya ligi mbalimbali duniani kupitia droo ya Perfect 12.

Mtalamu ambaye ni mkazi wa Kidatu, Kilombero mkoani Morogoro amekuwa mshindi wa nane wa droo hiyo tangu ilipoanza kuchezeshwa mwaka huu, amesema Meneja wa Masoko wa M-Bet Tanzania, Allen Mushi.

Meneja huyo alisema wanajisikia fahari kubwa sana kuendelea kuinua vipato vya Watanzania kupitia michezo yao ya kubahatisha. Washindi hao wanaingia katika orodha yao ya nyumba ya mabingwa.

Kwa upande wake, Mtalamu aliipongeza kampuni hiyo kwa kufanya shughuli zake kwa uwazi na kuwazawadia washindi zawadi zilizokamilika.

"Nimefarijika sana kushinda leo (jana), hizi fedha nitaanzisha biashara mpya huku nikiimarisha biashara yangu," alisema Mtalamu.

Wakati huo huo jumla ya washindi wanne wameshinda zawadi ya fedha katika mchezo mpya wa kubahatisha wa M-Bet unaotambulika kwa jina la Shinda Extra ambao ni Daniel Mbasha, Hamisi Victor na Jusiri Allem ambao kila mmoja amejishindia Sh. 500,000.

Kampuni hiyo imepanga kutumia zaidi ya Sh. milioni 18 kuzawadia washindi kupitia mchezo huo na wachezaji ambao wamejisajili kupitia App ya M-Bet watalipa Sh.500 huku wasiosajiliwa watalipa Sh. 1000.




Meneja Masoko wa Kampuni ya M-BET, Allen Mushi (kulia), akikabidhi mfano wa hundi ya Sh. milioni 78.2 kwa mshindi wa mchezo wa kubahatisha wa Perfect 12, Joel Mtaalamu kutoka Kidatu, Kilombero baada ya kubashiri kwa usahihi mechi 12 za ligi za mpira wa miguu mbalimbali duniani. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Michezo

Ijumaa Machi 6, 2021

Nipashe




KLOPP: LIVERPOOL MAMBO NI MAGUMU HABARI UK 22



Kiungo wa Simba, Jonas Mkude (kushoto), akiwania mpira dhidi ya kiungo mkabaji Mganda, Taddeo Lwanga kwenye mazoezi ya timu hiyo kwa ajili ya kujiandaa na mechi ya Kundi A ya Ligi ya Mabingwa Afrika itakayochezwa leo jijini Khartoum, Sudan. **PICHA: MTANDAO**

# SIMBA YAJIPANGA KUKAMILISHA KAZI

## ●●●Gomes afunguka watacheza kwa tahadhari na heshima dhidi ya klabu yake ya...

**Na Mwandishi Wetu, SUDAN**

SIMBA maarufu Wekundu wa Msimbazi kutoka Kariakoo jijini Dar es Salaam wanatarajia kupeperusha bendera ya Tanzania kwa kuwakabili wenyeji Al Merrikh katika mechi ya Kundi A ya Ligi ya Mabingwa Afrika itakayochezwa leo kwenye Uwanja wa Al Hilal ulioko jijini Khartoum nchini Sudan.

Mechi hiyo ni ya mzunguko wa tatu na Simba itashuka dimbani ikiwa na rekodi ya kushinda michezo yake miwili ya awali dhidi ya AS Vita ya Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC) na Al Ahly ya Misri.

Kocha Mkuu wa Simba Mfaransa Didier Gomes, ameliambia gazeti hili jana mechi hiyo itakuwa ngumu na yenye ushindani na kikosi chake kimejiandaa vyema kukabiliana na changamoto hiyo.

Gomes alisema watawavaa wapinzani wao kwa tahadhari kwa sababu wanajua hali ambayo wanakutana na timu iliyopoteza mechi zilizotangulia kwenye michuano hiyo.

Kocha huyo alisema kila mchezaji wa Simba yuko tayari kwa ajili ya kupambana kusaka matokeo mazuri ili kujiimarisha kwenye msimamo wa Kundi A na hatimaye kusonga mbele katika michuano hiyo.

"Si mechi rahisi, tunaenda kucheza na bingwa wa Sudan, hakuna ambaye anamdharau mpinzani wake, hii ni ligi ya mabingwa, hivyo wote tuna nafasi sawa kabla ya mechi kuanza, kikubwa ni kufuata mipango kuhusiana na mchezo huo," alisema Gomes.

Aliongeza wachezaji wote walioko Sudan wako fiti na tayari kukamilisha majukumu yaliyowapeleka nchini humo.

John Bocco, nahodha wa timu hiyo alisema wachezaji wako tayari kukamilisha kazi iliyowapeleka Sudan na wanachowaza ni ushindi pekee.

"Tuko salama, tuko tayari kufanya mambo mazuri kesho (leo), Jumamosi, tunajua ushindi utatuweka katika nafasi nzuri ya kutimiza malengo yetu," Bocco alisema.

Mkuu wa Idara ya Habari na Mawasiliano wa Simba, Haji Manara alisema mchezo wa kesho ni mkubwa na timu yao imejipanga kucheza kwa heshima na utulivu.

Manara alisema maandalizi yote muhimu kuelekea mechi hiyo yamekamilika na kila idara imefanya majukumu yake katika kiwango cha juu.

"Al Merrikh na Simba ni mechi kubwa, ni mechi ya mabingwa wa Afrika, tumekuja hapa kukamilisha kazi, hatujaja hapa kufurahishana, lakini vile vile hatujaja kuogopana, tutawaheshimu Al Merrikh bingwa wa Sudan, kama timu yenye uzoefu ukubwa, safari hii Simba tunaweza kupata ushindi popote, iwe nyumbani, iwe ugenini," alisema Manara.

Aliongeza kwa kuwataka mashabiki na wanachama wa timu hiyo kuzidisha maombi kwa timu yao ambayo imedhamiria kutangaza vizuri jina la Tanzania kupitia michuano hiyo ya kimataifa.

Hii itakuwa ni mara ya kwanza kwa Gomes ambaye alijiunga na Simba akitokea Al Merrikh kuiongoza timu hiyo kwenye ardhi ya Sudan huku Waarabu hao wakiwa hawajashinda mechi hata moja kwenye michuano hiyo.

Taarifa za awali kutoka Khartoum zinasema hali si shwari katika kambi ya Al Merrikh na endapo itapoteza mechi ya leo, hali itakuwa mbaya zaidi.

# MIKAKATI MIPYA YASUKWA YANGA

**Na Saada Akida**

WAKATI kikosi tayari kimewasili jijini Arusha, Kocha Mkuu wa Yanga, Cedric Kaze amesema timu yake ilistahili kupoteza mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara dhidi ya Coastal Union kutokana na wapinzani wao kuonyesha kandanda safi.

Kaze aliliambia gazeti hili timu yake haikucheza katika kiwango cha kuridhisha na hakuna yoyote wa kumtupia lawama kwa matokeo hayo ambayo yalimaliza utawala wa kutofungwa msimu huu.

Kocha huyo amesema tayari ameshayafanyia kazi mapungufu yaliyojitokeza kwa ajili ya kujiimarisha kuelekea mchezo ujao ambao watakuwa ugenini dhidi ya Polisi Tanzania kwenye Uwanja wa Sheikh Amri Abeid.

"Ninawapongeza wapinzani kwa kucheza vizuri na kutumia mapungufu yetu kutuadhibu, ni mechi yetu ya kwanza kufungwa tangu tumeanza ligi, hatuna kisingizo chochote ikiwamo uwanja, wala kumtupia lawama yoyote, bali kiwango chetu hakikuwa cha kuridhisha na sasa tunaenda kujipanga kwa ajili ya mechi ya Jumapili," alisema Kaze.

Aliongeza kikosi chake hakikuwa na bahati katika mechi hiyo huku akiwataja wachezaji watatu wanaopiga penalti kuwa ni pamoja na Tuisila Kisinda ambaye juzi alikosa, Michael Sarpong na Fiston Abdulrazaq.

"Niliwaambia vijana wangu kuwa mchezo utakuwa mgumu, tunacheza na timu kubwa, yenye wachezaji wazuri, wanapaswa wapambane ndani ya uwanja, niwapongeze wamefuata kile nilichowaelekeza na kubakiza pointi tatu nyumbani," Juma Mgunda, Kocha Mkuu wa Coastal Union alisema.

Mgunda alisema ushindi wa mabao 2-1 walioupata ulichagizwa na mchezaji wa 12 ambao ni mashabiki wao na kuweka rekodi ya timu ya kwanza kuifunga Yanga ndani ya msimu huu.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002